**MIAKA 3 YA SAMIA** Aja na vituo afya 485, Kenya wavuka mpaka kupata somo



UKURASA 4

**ASKOFU** Shoo alia msukumo mdogo marekebisho ya Sheria ya Ndoa

UKURASA 2

**SERIKALI** yajipanga majanga kemikali, nyuklia, radiolojia

UKURASA 3



**RAYA APIGIWA DEBE ARSENAL**

UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Machi 15, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581616

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@nipashe.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Kasi ya kuasili watoto yashtua



Takwimu na hodi zaipa kiulizo serikali... Endelea ukurasa wa 2

## VIGEZO ANAYEASILI MTOTO

01 Umri wake usizidi miaka 50

02 Awe na familia ya mke na mume

03 Awe raia wa Tanzania, athibitishwe kitabibu utimilifu afya ya akili

04 Polisi wamkague usafi wake dhidi ya makosa ya jinai

05 Familia iwe imeridhia kutekeleza utashi huo

06 Atume ombi rasmi kwa mwenye dhamana kiserikali

07 Ombi hilo litathibitishwa na mahakama kuidhinisha uhalali

# Kuuza gesi bila ya mizani, faini 300,000/- inakuhusu

UKURASA 5



Mchuuzi wa magimbi (kushoto), akimhudumia mteja wake katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Magimbi yanayotumika sana kutengenezea futari yamepanda bei kutoka 1,500/- hadi 2,000/- na 3,000/- kwa fungu moja hasa katika kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: JUMANNE JUMA**



**Simba tishio kwa binadamu wahamishwa**

UKURASA 8

**MICHEZO** **BENCHIKA: AL AHLY WANAIHOFIA SIMBA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Askofu Shoo alia na msukumo marekebisho Sheria ya Ndoa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

ASKOFU Mkuu mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo amesema jitihada za makusudi zinahitajika kwa wadau kushawishi watunga sheria kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu ndoa katika umri wa miaka 16 na kukinzana na Sheria ya Mtoto (2009) inayomtambua ni mwenye umri chini ya miaka 18.

Dk. Shoo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Mradi wa Hapana Marefu Yasiyo na Mwisho unaoratibiwa na KKKT, aliyasema hayo mjini Morogoro juzi alipozungumza na wajumbe wa kamati hiyo waliokuwa wanafanya tathmini ya mwaka mmoja wa utekelezaji wake.

Alisema bila jitihada za makusudi, mtoto ataendelea kuolewa katika umri mdogo na kubeba majukumu makubwa ya kifamilia asiyo na uwezo nayo. Ikiwa watunga sheria wataliona jambo hilo, watakubali kurekebisha sheria.

Kwa mujibu wa Askofu Shoo, mradi huo unalenga kuleta mabadiliko chanya katika mila potofu na kandamizi zinazochangia kuendelezwa ukatili wa kijinsia na kutokomeza ndoa za utotoni.

Askofu Shoo alisema upo umuhimu mkubwa siyo tu kwa viongozi wa dini, bali pia viongozi wengine wakiwamo wa kiserikali, kimila na kisiasa ambao ndio wafanya uamuzi, kuweka nguvu za pamoja kuhakikisha utamaduni, tabia ya ndoa za utotoni zinazomnyima fursa mtoto wa kike kukua na kuendeleza vipaji vyake zinakoma kwa kuwa zinamnyima kuwa mama bora, anayejiamini, mwenye maarifa na mwenye uwezo kulea jamii.

"Kwa pamoja na kwa nia njema, tuangalie upya sheria hii na watunga sheria wafanye mabadiliko dhidi ya sheria hii ili zisikinzane na ile ya ulinzi wa mtoto, kila mtu anapenda kuona mabinti wote wa kitanzania wanapata haki sawa na wanaume, usichopenda binti yako atendewe, usitake na wa mwingine afanyiwe, chukia hali hiyo," alisema Askofu Shoo.

Mratibu wa mradi huo, Patricia Mwaikenda alisema kikao hicho kimelenga kupokea utekelezaji mradi huo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita tangu Aprili Mosi, 2023 hadi Machi 30, mwaka huu na kupokea mpango kwa ajili ya mwaka mwingine ujao.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Zanzibar, Anna Athanas Paul alisema Sheria ya Ndoa kwa upande wao hawajaifanyia mchakato wowote kwa sababu wanasimamia zaidi Sheria ya Mtoto Na. 6 ya Mwaka 2011 ambayo inamtambua mtoto ni mwenye umri chini ya miaka 18 na kumpa haki zote ikiwamo kusoma, kutunzwa na wazazi wake, kulindwa na haki nyingine nyingi.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Linus Kahendaguza alisema ofisi yao imeendelea kuhakikisha watoto walio shuleni na nje ya shule wanakuwa salama na kufikia ndoto zao bila kuwa na vizuizi vya kuolewa wakiwa watoto.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
14.03.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **18.03.2024 hadi 24.03.2024 kampuni ya CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar es salaam** kuelekea **Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | Mita | 28.0 |
| Upana | - | Mita | 5.5 |
| Kimo | - | Mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga** kupitia **Barabara ya Morogoro,** gari litasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

117878402

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***





Mshindi wa bajaji katika droo ya kwanza ya kampeni ya Benki ni Simbanking inayoendeshwa na Benki ya CRDB, Adam Salehe Rashid akionyesha funguo baada ya kukabidhiwa zawadi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki hiyo, Stephen Adili (wa pili kulia), huko Chanika, jijini Dar es Salaam jana. **Habari Uk. 5.** **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kasi kuasili watoto yashtua

**Na Halfani Chusi**

KUNA ongezeko kubwa la watu wanaotaka kuasili watoto nchini kwa sasa, serikali imethibitisha.

Maofisa Ustawi wa Jamii wamesema ongezeko hilo linasababishwa na kuongezeka kwa watu wenye changamoto za uzazi, hivyo kulazimika kuasili watoto.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Nyamala Elisha, ndiye amebainisha hali hiyo, akieleza kuwa kwa sasa kuna wimbi kubwa la watu wanaokwenda katika ofisi hizo za umma kwa lengo la kuasili watoto kutokana na changamoto za uzazi zinazowakabili.

Ni alipomwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam katika mahafali ya kwanza ya Chuo cha Biashara Kibaha yaliyofanyika Mburahati, wilayani Kinondoni. Wahitimu wote walifadhiliwa na Serikali ya Canada iliyoshirikiana na shirika la World Vision Tanzania.

Akirejea taarifa za ofisi yake, Elisha alibainisha kuwa kipindi cha nyuma, ulikuwa unapita mwezi mzima pasi na kupokea hata mteja mmoja anayehitaji kuasili mtoto, lakini sasa wana wastani wa kupokea mmoja hadi wawili kila mwezi huku wakipokea wastani wa simu tatu hadi nne toka kwa wanaohitaji kujua taratibu za kuasili mtoto.

Elisha pia alionya wazazi wanaotweza utu wa watoto kwa kuwatupa, kuwatelekeza na kuwafanyia vitendo vya kikatili, akisisitiza watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Wakati wewe unatupa mtoto wako, yupo ambaye anamtafuta kwa muda mrefu na hampati. Moja ya changamoto kubwa inayotutesa ni kwenye malezi ya watoto; tunawalea vibaya, wanakua kwa kudra za Mwenyezi Mungu.

"Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, imetoa rukhsa ya kuasili mtoto na atahesabika ni wako kama ambavyo ulipata bahati ya kumzaa mtoto isivyo ridhiki.

"Kwahiyo, mtoto huyo atakuwa ni wako, atarithi kila kitu na ataitika ukoo wako. Kuanzia hapo utakuwa umetengeneza ukoo kama ambavyo ungeweza kumpata kwa njia ya kawaida kutokana na kudra za Mwenyezi Mungu.

"Hatuwezi kumhoji Mwenyezi Mungu 'kwanini wengine wanakosa?' lakini wakati hawa wanapitia hayo, wanahangaika barabarani mara kwa mwanasheria, mara nenda Dodoma zaidi ya miaka miwili mpaka mitatu kwa ajili ya kupata mtoto, wapo wanaotelekeza watoto, inauma sana," Elisha alisema kwa hisia.

Ofisa Ustawi wa Jamii huyo pia alielekeza watumishi wa umma kuweka kipaumbele kusaidia watoto watimize ndoto, hasa kuingia mtaani kukumbusha jamii kuhusu umuhimu wa malezi na makuzi ya mtoto.

**VIGEZO KUASILI**

Elisha alitaja vigezo anavyopaswa kutimiza mtu anayehitaji kuasili mtoto ni pamoja na kuwa na umri wa kuanzia miaka 25 na usiozidi miaka 50 (kama anazidi miaka 50, aasili mtoto mwenye umri wa kuanzia miaka 10); awe na familia ya mke na mume; awe raia wa Tanzania; awe na fomu kutoka kwa daktari wa afya ya akili inayothibitisha utimamu wake na awe na fomu ya polisi inayothibitisha hajawahi kufanya jinai yoyote.

"Baada ya hapo tunapeleka taarifa zake kwa Kamishina wa Ustawi wa Jamii Dodoma kumwambia kama tumejiridhisha na taarifa zake.

"Lakini pia atatakiwa awe na taarifa ya familia ambayo wameridhia, atatakiwa kufika mahakamani kwa ajili ya kuidhinisha na baada ya hapo tutamkabidhi mtoto na hatotakiwa kumfanyia vitendo vya ukatili na akifanya hivyo atachukuliwa hatua kama vile wanavyochukuliwa waliozaa kwa njia ya kawaida," alifafanua.

Kuhusu mahafali hayo, Elisha aliwataka wahitimu hao kutumia ujuzi waliopata chuoni kuajiri na kujiendeleza kibiashara, huku akiahidi kuangalia namna ya kundi hilo la vijana wenye umri chini ya miaka 18 kupata mikopo itakayowawezesha kujiajiri na kusaidia taifa kupiga hatua.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Biashara Kibaha, Antipas Kuyonza alisema walengwa wakubwa katika mradi huo ni vijana wanaotoka familia zenye maisha magumu.

Kuyonza alisema chuo hicho kinatoa mafunzo ya ujasiriamali, utunzaji fedha binafsi na biashara, jinsi ya kutafuta kazi na kutekeleza majukumu kwa weledi na kutoa mafunzo shirikishi kutoka kwa maofsa wa benki na manispaa za ndani.

Alisema wahitimu hao walianza masomo yao Septemba mwaka jana wakiwa 48 wakitoka katika kata tisa za manispaa nne za Mkoa wa Dar es Salaam. Kati yao, 45 wamehitimu, watatu waliacha kutokana na alichokitaja kuwa "sababu za kijamii".

"Waliopata fani ya umeme ni watano, mapishi na hoteli wako 15, saluni na ususi tisa, udereva sita, ufundi magari wanne ushonaji watano na uchomeleaji mmoja, lakini wote kwa ujumla wao walipata mafunzo ya kuandaa andiko la biashara," alibainisha.

Mkurugenzi Mwandamizi wa Shirika la World Vision Tanzania, Dk. Joseph Mayala, alisema shirika hilo limekuwapo nchini kwa zaidi ya miaka 40 sasa, likilenga kuleta maendeleo kwa watoto wa Tanzania.

HABARI KITAIFA

# Serikali yajipanga majanga kemikali, nyuklia, radiolojia

**Na Restuta James**

MAJANGA yanayotokana na bidhaa za kikemikali, kibaiolojia, kiradiolojia na kinyuklia, yameundiwa mpango wa kuyakabili huku wizara na taasisi za serikali zikielekezwa kushirikiana ili kutekeleza mpango huo.

Aidha, serikali imeandaa mpango wa kitaifa wa kukabiliana na vitisho vya kikemikali, kibaiolojia, kiradiolojia na kinyuklia na mpango wa kitaifa wa kujiandaa na kukabiliana na dharura za kinyuklia na kiradiolojia.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizindua nyaraka hizo za usimamizi wa maafa na kushuhudia zoezi la utayari wa kukabiliana dharura za kikemikali na kimionzi nchini.

Alisema lengo la kuwa na mpango huo ni kuiweka nchi katika hali ya utayari wa kukabili majanga hayo ili yakitokea madhara yadhibitiwe katika hatua za awali.

"Nazielekeza wizara na taasisi zote zinazohusika toeni ushirikiano unaohitajika na mfanye ufuatiliaji na tathmini ya utayari ili uwezo wetu wa kukabili majanga haya uwe endelevu," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu pia aliwataka wataalamu kutengeneza muundo wa ujenzi wa kituo kimoja cha mwitiko wa dharura wa majanga hayo, ambacho kitaratibu matishio ya kikemikali, kiradiolojia na kimionzi.

Amezielekeza idara zinazohusika na usafirishaji wa mizigo zikiwamo vituo vikubwa vya mabasi na viwanja vya ndege kuhakikisha vinafanya ukaguzi wa kina wa mizigo, ili kuiepusha nchi na majanga hayo.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Christine Grau, alisema nchi zinazounda Jumuiya hiyo, ziko tayari kushirikiana na serikali katika kukabili majanga ya kikemikali.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema mradi huo unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), ambao umetoa vifaa vya maabara, vya uokozi na kukabili majanga hayo vyenye thamani ya Sh. bilioni sita.

Alisema kwa Afrika, nchi 28 zinazoendelea na mradi huo na Tanzania imetajwa kufanya vizuri katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na kwamba watumishi waliopata mafunzo wako tayari kukabili majanga hayo wakati wowote.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomu (TAEC), Prof. Lazaro Busagala, Tanzania ilijiunga na mtandao wa kukabili majanga hayo mwaka 2014 na mwaka 2018 ikaunda timu ya kitaifa kuratibu matukio hayo. "Mradi huu umetupatia vifaa vya maabara vya kutambua na kuzuia hatari za majanga haya. Tayari watumishi 68 kutoka wizara na taasisi za serikali wakiwamo polisi, zimamoto, ofisi ya mkemia mkuu wa serikali, TAEC, Mamlaka ya Bandari (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu," alisema Prof. Busagala.

Alisema mafunzo hayo yamewezesha kuwepo kwa timu ya utambuzi wa janga na kulikabili katika hatua ya awali, kubainisha, kuchukua sampuli na kusafisha eneo la janga ili kuzuia madhara zaidi.

# Mbaroni tuhuma utapeli wa kutumia majina ya viongozi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawahoji watuhumiwa watano wakiwamo wawili wanaodaiwa kusambaza taarifa za uongo za uchochezi za kumng'oa Rais Samia Suluhu Hassan mwaka 2025.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kumiliki televisheni ya mtandaoni iliyotambulika kwa jina la Jamii Digital na akaunti ya mtandao wa X iitwayo SUKUNUNU 01.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana, alitaja watuhumiwa hao wawili ni Obadia Kwitega (35), mkazi wa Kigamboni na Issa Mwamba (28), mkazi wa Tabata Segerea, jijini.

Alisema watuhumiwa hao wanamiliki televisheni za mtandaoni ambazo huzitumia kusambaza taarifa za uongo na za uchochezi kuhusu viongozi wakuu wa serikali.

"Baadhi ya taarifa zao zinasomeka 'MKAKATI WA SIRI JANUARY MAKAMBA KUMNG'OA RAIS SAMIA 2025'," alisema.

Kamanda Muliro alitaja watuhumiwa wengine wa makosa ya mitandao wanaowashikilia ni Frank Mbetu (35), mkazi wa Ligula, Mtwara.

Alisema Mbetu anatuhumiwa kujifanya mtumishi wa serikali ngazi ya Katibu Mkuu Kiongozi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kuwa angewapa watu kazi serikalini au kupandishwa vyeo.

"Mtuhumiwa Honest Mgona (47), mkazi wa Mabwepande, amekuwa akijipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kuwa ametumwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Nchengerwa, kusambaza mitungi ya gesi kwa wananchi na baadaye kuwatapeli kwa kuwadai fedha za usafiri," alisema.

Kamanda Muliro alimtaja mwingine ni Edwin Kasebele (24), mkazi wa Mapelele, mkoani Mbeya, anayetuhumiwa kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa kijamii wa 'Facebook' na 'Whatsapp' kuwa anafanya biashara ya vitenge na kujipatia fedha kwa udanganyifu kutoka kwa watu mbalimbali.

Alisema watuhumiwa hao wamekutwa wakiwa na simu saba na kadi za simu 13 za kampuni za simu mbalimbali ambazo wamekuwa wanatumia kama nyenzo kutekeleza uhalifu wao.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alisema jeshi hilo linachunguza tukio la kuuawa mtoto wa miaka saba ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kibonde Maji B Mbagala na mwili wake kukutwa juzi katika msitu wa jeshi karibu na shule aliyokuwa anasoma.

Alisema taarifa walizozipata zinadai kuwa siku moja kabla ya tukio hilo, mtoto huyo aliondoka nyumbani kwao na mwenzake majira ya 11:30 jioni.

"Mwili wa marehemu umehifadhiwa Hospitali ya Polisi Kilwa Road kwa uchunguzi zaidi. Ufuatiliaji unaendelea kumtafuta mtuhumiwa au watuhumiwa waliohusika ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao," alisema Kamanda Muliro.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TAARIFA KWA WALIPAKODI WOTE

**Dar es Salaam, 12 Machi, 2024:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha Walipakodi wote kuwa, mwezi huu wa Machi ni wakati wa kulipa kodi ya awamu kwa kutumia mifumo ya ulipaji kodi iliyorahisishwa.

Kwa wafanyabiashara wanaojikadiria, wanaweza kuwasilisha ritani, kulipa kodi pamoja na madeni ya nyuma kwa njia ya mtandao kupitia lango la Mlipakodi (Taxpayer Portal) inayopatikana katika tovuti ya TRA **https://taxpayerportal.tra.go.tz/#/.**

Kwa wafanyabiashara wanaokadiriwa, wanasisitizwa kufika katika ofisi ya TRA iliyopo karibu ili kufanya makadirio na kulipa kodi zao kwa wakati.

Kumbuka, awamu hii kodi inalipwa kabla au mnamo **tarehe 31 Machi, 2024.**


Kwa maelezo zaidi, piga simu bure **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016.** Barua pepe: **huduma@tra.go.tz,** WhatsApp **0744-233 333.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**IDARA YA ELIMU KWA MLIPAKODI NA MAWASILIANO**

117876402



Rais Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na Mama Fatma Karume Mjane wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume baada ya kuzindua Chama cha Wanawake Sekta ya Fedha Tanzania (TAWiFA), Kizimkazi, Zanzibar jana. PICHA: IKULU

KUELEKEA MIAKA 3 YA RAIS SAMIA

# Amehakikisha sekta ya afya inatekeleza kila Mtanzania kuwa na afya bora

**Na Mary Geofrey**

ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/15 Ibara ya 81, imebainisha kuwa huduma za afya ni muhimu kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora, ili washiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anatekeleza ilani ya chama hicho, sekta ya afya imetekeleza mambo mbalimbali kwa kasi.

Hata hivyo, bado kuna changamoto ya vitita vipya vilivyotangazwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Bima ya Afya kwa wote, hali inayowarudisha mezani watoa huduma wa sekta binafsi na serikali.

**VITUO VYA AFYA 485**

Miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, vituo vipya 485 vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kutoka 8,881 Disemba 2022 na kufikia 9,366 Disemba 2023 sawa na ongezeko la asilimia 5.5.

Januari 10, mwaka huu, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, alitoa taarifa ya hali ya utoaji huduma za afya nchini kwa mwaka 2023.

Aidha, mgawanyo wa vituo hivyo vipya vya kutoa huduma za afya hadi kufikia Disemba 2023 ni pamoja na zahanati 7,804 sawa na asilimia 83.3, vituo vya afya 1,126 sawa na asilimia 12.02, hospitali za halmashauri 171 sawa na asilimia 1.83 na hospitali zenye hadhi ya wilaya 180 sawa na asilimia.

Pia, hospitali za rufani za mikoa 28, zenye hadhi ya mkoa (34), rufaa za kanda (5), hadhi ya kanda (11), maalumu sita na Hospitali ya Taifa moja.

"Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini limetuwezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi kama tunavyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/25," anasema Ummy.

**HUDUMA ZA KIBINGWA**

Katika kipindi chake amezindua huduma katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara, ikiwapo mashine ya CT Scan na X Ray tatu ambazo zote hizo zinagharimu Sh. bilioni 7.5.

Amehakikisha fedha zote za dawa zinatoka kwa asilimia 100 na kutoa Sh. bilioni 17 kwa ajili ya ujenzi wa Bohari ya Dawa Kanda ya Kusini na ujenzi wake tayari umeanza.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Mollel ananukuliwa akisema, kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetoa Sh. bilioni 22 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mtwara, kwaajili ya ujenzi ambao upo katika hatua za mwisho za kukamilika.

Aidha, tayari sekta ya afya ametoa Sh. tilioni 6.7 ambayo imefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya nchini kwa kununua CT Scan 32, X Ray za kisasa 199 na kufanya nchi kuwa na jumla ya X Ray 543.

"Hivyo kwa mtu aliyeko Tandahimba, Newala akipata Huduma ya X Ray tuna uwezo wa kuunganisha na kusoma majibu yake kwa kutumia X Ray za kisasa zilizosimikwa katika hospitali zote," anasema Dk. Mollel.

Kuwapo kwa uwekezaji huo upande wa Kanda ya Ziwa, kunapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wagonjwa wanaosafirishwa kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

**KENYA YAJIFUNZA NCHINI**

Kutokana na mageuzi makubwa yanayoendelea katika sekta ya afya nchini, Serikali ya Kenya ilituma wataalam wake kuja nchini Tanzania kujifunza namna sekta ya afya umefanikiwa kupiga hatua kubwa za matibabu ya kibingwa.

Waziri wa Afya kutoka Kenya, Peter Samwel Mwarogo, akiwa na Wabunge wa Kamati ya Afya ambao walitembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili mapema mwaka huu, walitaka kuona mageuzi kupitia huduma, uwekezaji vifaa tiba, uboreshaji miundombinu na utawala.

"Tumekuwa tukisikia maboresho ya huduma Tanzania hususani Hospitali ya Taifa Muhimbili, hivyo tumekuja kujifunza mambo mengi mtambuka ili tukaboreshe sekta ya afya kwa ujumla wake katika jimbo letu," anasisitiza Mwarogo.

Pia, wamejifunza kuhusu uendeshaji wa mtambo wa kuchoma taka, kliniki za wagonjwa wa kulipia, uwajibikaji wa watumishi, idara ya dharura, radiolojia na masuala mengine.

**KITUO CHA MATIBABU SARATANI**

Serikali pia imeahidi kuendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya vituo vya afya pamoja na kuweka mikakati inayolenga upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote ili kuimarisha kinga na tiba ya maradhi ya saratani.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa kwenye kikao cha wadau wa uwekezaji na maendeleo kwaajili ya uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri wa Matibabu ya Saratani nchini, anasema kituo hicho kitakuwa pekee cha umahiri wa matibabu ya saratani katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Maradhi ya saratani ni ugonjwa unaoathiri mamilioni ya watu kote ulimwenguni, hivyo kama jamii tunapaswa na sisi kuwekeza katika kinga na tiba ya maradhi haya, tayari serikali imeanza kuchukua hatua na tunashuhudia hatua katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya na mikakati inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za matibabu kwa wote," anasema Dk. Mwinyi.

**VIPAUMBELE SITA VYA KISERA**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imebainisha vipaumbele sita vya kisera katika sekta ya afya ambavyo vitawekewa mkazo zaidi katika kutekelezwa kwa mwaka 2024/25, ili kuendelea kuboresha huduma za afya nchini.

Waziri wa Afya, Ummy, alikuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka wa kisera wa 23 wa sekta ya afya uliofanyika jijini Dodoma Februari 15, mwaka huu.

"Serikali imejitolea kuwekeza katika mafunzo na maendeleo ya watumishi wa afya ili kuhakikisha huduma bora zinapatikana kwa wananchi," anasema Ummy.

Vipaumbele hivyo ni pamoja na rasilimali watu katika afya, ubora wa huduma, utekelezaji wa sheria ya bima ya afya kwa wote, wahudumu wa afya ngazi ya jamii, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza na kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika utoaji huduma za afya.

**BIMA YA AFYA KWA WOTE**

Kwa sasa Tanzania kuna Sheria ya Huduma ya Afya kwa Wote iliyokwisha kupitishwa na Bunge ikisubiri kanuni ili ianze kutekelezwa, kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya.

Kupitia NHF taratibu za kuanza kutoa huduma za bima ya afya kwa wote na hatua ambayo imeshaanza ni mwongozo uliotolewa na serikali wa huduma za vifurushi vipya kwa vituo vya kutoa huduma za afya nchini.

# Apelekwa jela miaka mitano kutoroka mahabusu ya polisi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Dodoma imemtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitano gerezani Daniel Simle baada ya kukiri kosa la kutoroka akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi.

Simle anadaiwa kumnajisi kwa miaka mitatu mfululizo binti yake mwenye umri wa miaka 10 sasa.

Mshtakiwa huyo alitiwa hatiani juzi mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, Francis Kishenyi baada ya kukiri kosa la kutoroka akiwa chini ya ulinzi.

Wakili wa Serikali Francis Kesanta, akisoma mashtaka hayo, alidai kuwa Julai 30, mwaka jana, mshtakiwa alitoroka akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi wa Kituo cha Polisi Mvumi, wilayani Chamwino, alikoshikiliwa wakati uchunguzi wa tuhuma za kunajisi mwanawe ukiendelea.

Baada ya kusomewa maelezo yanayojenga kosa lake kwenye kesi hiyo, mshtakiwa Simle alikiri kutenda kosa hilo.

"Kutokana na kukiri kwake kosa, mahakama imemwona mshtakiwa ana hatia, hivyo inamhukumu kifungo cha miaka mitano jela," Hakimu Kishenyi alisema.

Nje ya mahakama, Wakili wa Serikali Mwandamizi Mkoa wa Dodoma, Lina Magoma, alisema wanakamilisha taratibu za kisheria kumfungulia Simle kesi ya pili ya kunajisi mwanawe.

Baada ya kusakwa na polisi kwa siku 189 kutokana na kutoroka mahabusu ya polisi wilayani Chamwino, Simle alikamatwa jijini Dar es Salaam Februari 6, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kituo cha Polisi Tabata, David Mwakinyuke, Simle alikamatwa na walinzi shirikishi - sungusungu waliomwekea mtego kisha wakampeleka kwenye kituo hicho cha polisi na hatimaye kusafirishwa kurejeshwa Chamwino, Dodoma.

# Kuuza gesi bila ya mizani, faini 300,000/- inakuhusu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAFANYABISHARA wa gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani wametakiwa kuwa na mizani sehemu wanazouza nishati hiyo itakayo hakikisha mteja anapata bidhaa kwa uzito anaoulipia.

Mmoja wa wakazi wa mtaa wa Kihonda mkoani hapa, Paulina James alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari kutokana na wauzaji wa nishati hiyo kutopima uzito wa mitungi inayojazwa gesi na kuwapunja wateja.

"Nilishawahi kununua gesi kwenye mtungi wa kilogramu 15 ambao huwa nautumia kwa nusu mwezi au mwezi kasoro, lakini nilitumia kwa siku sita hadi nane na mtungi ukawa umekwisha, nikashindwa kuelewa tatizo linatoka wapi, lakini baada ya kupata elimu kuwa wanaouza mitungi ya gesi wanapaswa kuwa na mizani nikaona ni jambo jema kwa ajili yetu," alisema James.

Aidha, aliiomba serikali kuweka msimamo katika kusimamia suala la matumizi ya mizani kwa wauzaji wa gesi kwa sababu baadhi ya wauzaji huuza mitungi yenye nishati pungufu na kumpunja mnunuzi kitendo kinacho haribu mipango yake ya bajeti.

Meneja wa Wakala wa Vipimo na Mizani (WMA), Mkoa wa Morogoro, Phanuel Mtuki, aliwataka wauzaji wa mitungi ya gesi ya matumizi majumbani lazima wawe na mizani wakati wa kuwauzia wateja ili kuepusha udanganyifu kwa wateja.

Mtuki alisema kisheria muuzaji wa gesi anapaswa kuwa na mzani wa kupimia mtungi wa gesi kabla ya kuuza na akikutwa anafanya biashara bila kuwa na mzani atalazimika kulipa faini ya Sh. 300,000 kama adhabu au kufungiwa biashara yake.

Aidha, aliwataka wanunuzi wa nyama na samaki kwenye mabucha kuwa makini na baadhi ya wauzaji wanaotumia mbinu mbalimbali kufanya udanganyifu kwa kuuza pungufu.

"Hakikisha hununui nyama au samaki kwenye bucha ambalo feni inawaka, kisheria feni ina nafasi ya kuongeza uzito kwenye mzani na hivyo mnunuzi anaweza asipate halali ya alichonunua, na zipo mbinu nyingi ambazo hufanywa na wauzaji, kuweni makini, na mkimkuta muuzaji wa hivyo ukamwambia anakubishia njoo utoe taarifa tumchukulie hatua haraka" alisema Mtuki.

Alisema WMA inaendelea kukemea tabia za kudhulumu wateja kwa kutoa adhabu kuanzia Sh. 300,000 hadi Shilingi milioni moja kupitia sheria mbalimbali.

Mmoja wa wauzaji wa gesi kwenye eneo la Mji Mpya, Muhidin Aminieli aliwataka wanunuzi wa gesi kuwa na matumaini na wauzaji wa mitungi ya gesi kwa sababu hawawezi kuwaibia pia kwa sasa wanatumia mizani kwa mujibu wa sheria.

# Benki yakabidhi bajaji, pikipiki kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA watatu wa Benki ya CRDB wamekabidhiwa zawadi zao baada ya kuibuka washindi kutokana na kufanya miamala mingi ya huduma za benki kupitia simu zao za mkononi, maarufu Simbanking.

Akikabidhi zawadi hizo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili alisema huo ni mwanzo tu kwa wateja wa benki hiyo kujinyakulia zawadi katika promosheni yao ya mwaka mzima ya Benki ni Simbanking.

Adili alisema teknolojia imerahisisha mambo mengi hivi sasa kwa kuwawezesha wateja kupata huduma kupitia majukwaa tofauti zikiwamo simu za mkononi ambazo kwa benki hiyo inayo Programu ya Simbaking inayowaruhusu kupata zaidi ya asilimia 95 ya huduma zake mahali popote walipo.

"Simbanking imedumu sokoni kwa zaidi ya miaka 15 sasa, ni njia rahisi ya kupata huduma za benki na kwa sasa tunayo kampeni ya kuhamasisha wateja wetu na wananchi kwa ujumla kuitumia na wale wanaoitumia zaidi tunawapa zawadi za aina tofauti.

"Leo (jana) tupo hapa Chanika (Ilala) kukabidhi bajaji moja na pikipiki kwa washindi wetu waliopatikana katika droo ya kwanza ya kila mwezi," alisema Adili.

Waliokabidhiwa zawadi hizo ni Adam Rashid aliyejishindia bajaji pamoja na Kibwana Kilongo na Rahma Kyalumbika walioshinda pikipiki kila mmoja. Kukabidhiwa kwa zawadi hizo kunakumbusha wateja wengine wa Benki ya CRDB kuendelea kutumia Simbanking hali itakayowaweka kwenye nafasi ya kushinda pikipiki au bajaji nyingine zitakazokuwa zinatolewa kila mwezi au gari aina ya Toyota Dualis itakayoshindaniwa kila baada ya miezi mitatu.

"Washindi hawa watatu wa kwanza wamefungua pazia kwa mwaka huu. Ninaomba mfahamu kwamba kuna magari manne aina ya Toyota Dualis yanayoendelea kushindaniwa, hivyo ninawasihi wateja wetu na watanzania ambao hawatumii huduma zetu, basi wafungue akaunti kwani kwa kufanya hivyo tu watakuwa wanaingia kwenye droo ya kushinda moja kati ya zawadi nyingi tulizonazo," alisema Adili.

Alisema kuwa ili kushinda moja ya zawadi zinazotolewa na Benki ya CRDB, mteja anatakiwa kufanya miamala mingi kupitia Simbanking kama vile kulipia bili za umeme na maji, kukata tiketi ya usafiri wa ndege, kulipa ada na michango ya shule, kulipia bidhaa zinazouzwa mtandaoni au kununua muda wa maongezi na huduma nyingine nyingi zinazopatikana ndani ya Programu ya Simbanking.

"Sifa zilizowapa ushindi wateja hawa watatu zinawezekana kwa mteja mwingine yeyote wa Benki ya CRDB, hivyo niwahimize wateja wetu wote kutoka mahali popote walipo kuendelea kutumia huduma za Simbanking ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kushinda zawadi kemkem tulizonazo," alisema mkuu huyo.

Akipokea pikipiki yake, Rahma alisema ataifanya bodaboda ili imwingizie kipato.

"Naamini haitonifaidisha peke yangu. Dereva atakayekuwa anaiendesha naye atapata kitu cha kuisaidia familia yake. Nimefurahi kushinda na ninaipenda zaidi Benki ya CRDB kwani inarudisha sehemu ya faida yake kwetu," alisema.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**IMERUDIWA: MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI HUDUMA YA UCHUKUAJI WA KUMBUKUMBU ZA PICHA ZA MNATO NA VIDEO KWA AJILI YA KAMPUNI YA EACOP LTD NCHINI TANZANIA KUMBUKUMBU NA: 00000437**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya kumbukumbu za Picha za mnato na Video kwa ajili mradi wa EACOP nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 196 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya Uchukuaji wa kumbukumbu za Picha za mnato na Video kwa ajili mradi wa EACOP nchini Tanzania.

- Kutoa huduma za kitaalamu za upigaji picha za mnato kulingana na mahitaji ya kampuni.
- Kutoa huduma za upigaji picha za video, ikijumuisha utayarishaji wa video na uhariri.
- Kujumuisha jumbe na chapa ya kampuni katika maudhui ya video.
- Kushiriki katika uundaji maudhii na ubunifu wa mawazo yanayowiana na chapa ya kampuni.
- Kuandaa vibali muhimu na ruhusa kwa ajili kutayarisha video katika maeneo lengwa.
- Kutangaza matukio ya kampuni, makongamano na warsha.
- Kupiga picha za matukio muhimu na kutoa mchanganyiko wa picha halisi katika mionekano mbalimbali ya kuvutia.
- Kupiga picha za kitaalamu za sehemu ya uso wa kampuni na wana timu.
- Kufanya usanifu baada ya utayarishaji, ikijumuisha urekebishaji wa rangi na uhariri
- Kupanga na kuhifadhi nyaraka za kidijitali kwa usalama kwa ajili ya matumizi ya kampuni.
- Kuwezesha wasomaji wa majukwaa ya mtandaoni kutazama na kupakua mafaili.

**VIGEZO MUHIMU:**

***Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:***

- Maelezo ya uzoefu, utalaamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda yanayohitajika.
- Maelezo ya kampuni yanahusu huduma zinazotolewa, uthibitisho wa utendaji kazi, pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu walikwisha fanya kazi na kampuni hiyo.
- Leseni ya biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha kivuli cha cheti).
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya watoa huduma za ugavi wa ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya ndani.
- Uthibitisha wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa mifumo ya usimamizi wa shirika la QHSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani ni viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Makampuni yenye nia, yenye uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **29 Machi 2024** saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) Kichwa cha Barua pepe kiwe: **00000437** Utoaji huduma ya kumbukumbu za Picha za mnato na Video. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

117877702

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wazingatie maagizo ya Rais kuhusu misingi inayotakiwa

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi aliwaapisha baadhi ya viongozi aliowateua hivi karibuni katika ngazi mbalimbali huku akiainisha mambo kadhaa zikiwamo sababu za kuteua na kutengua baadhi ya wateule wake. Miongoni mwa wateule walioapishwa ni wakuu wa mikoa na naibu katibu mkuu mmoja.

Pamoja na kutoa sababu hizo, Rais Samia katika hafla hiyo iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam, aliweka wazi kwamba hana mtu anayemkumbatia na kuwataka wateule hao kuwajibika ipasavyo katika nafasi zao.

Rais Samia katika ujumbe wake huo, alitoa msimamo wake ndani ya chama kinachotawala- Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho yeye ni mwenyekiti wa taifa na serikali anayoiongoza kwamba yeye ni mtu wa watu wote na asiwapo mtu anayedhani kwamba anambeba, hivyo anaweza kufanya awezavyo na asichukuliwe hatua.

Pia alibainisha kwamba hana kundi ndani ya serikali na chama, hivyo anapofanya uteuzi anaangalia sifa na si makundi ya wateule hao. Kutokana na ukweli huo, alisema hata mabadiliko anayoyafanya mara kwa mara ambayo pia husababisha baadhi ya watu kuondolewa kwenye nafasi zao, hayalengi makundi wala upande wowote.

Mbali na kuweka msimamo huo, Rais Samia alionyesha kukerwa na baadhi ya viongozi katika ngazi mbalimbali, kwa kutumia nafasi zao, kuvunja mikataba ambayo iko kisheria, hivyo kusababisha serikali kuingia hasara kwa kulipa mabilioni ya fedha pindi inaposhtakiwa kwa vitendo hivyo.

Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, aliwataka viongozi wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya ambao wameelezwa kuwa chanzo cha kufanya hivyo, kufuata sheria kanuni na taratibu. Aliwataka kutambua kuwa mikataba hiyo imeingiwa kisheria, hivyo hatua ya kuvunja inaweza kuliingiza taifa katika hasara kama ambavyo imetokea katika baadhi ya maeneo.

Aidha, Rais Samia aliweka bayana kwamba kuna wizi na udokozi katika serikali na taasisi zake hasa kupitia mifumo ya ukusanyaji mapato, akitolea mfano wa mitandao ya uchepushaji fedha za halmashauri, mkoa ambao unashirikiana na viongozi wa serikali lakini wateule wake wanaangalia tu.

Kuwapo kwa mtandao huo wa wizi wa fedha za umma, Rais alisema unahatarisha kuzorota kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama vile elimu, afya, kilimo, barabara, maji na ujenzi wa miundombinu mingine hali ambayo inasababisha wananchi kuendelea kuwa katika lindi la umaskini na changamoto zisizopatiwa suluhisho miaka nenda rudi.


Kutokana na kuwapo kwa matatizo hayo, Rais aliwataka wateule hao kwenda kusimamia na kutatua kero za wananchi kama ilivyobainika katika ardhi ambako kuna migogoro mingi ambayo baadhi inahusisha viongozi na maofisa waliopewa dhamana ya kusimamia sekta hiyo.

Kauli hiyo ya Rais kuhusu watu kutumia nafasi zao vibaya, wizi na kero zinazowakabili wananchi si mara ya kwanza kuitoa. Amekuwa akiitoa mara kwa mara akiwa anazungumza na wateule baada ya kuwaapisha na kuwataka wakasimamie misingi ya uongozi pamoja na kanuni na taratibu. Licha ya kuwaeleza mara kwa mara, matatizo yamekuwa yakiendelea kila uchao, hivyo kudhihirisha kwamba watu hao hawaendi kufanya yale wanayoelekezwa.

Kwa jumla, Rais amezungumza sana kuhusu wajibu wa viongozi anaowateua lakini wamekuwa kama watu wenye masikio yasiyopokea na kutekeleza maagizo hayo. Kwa maneno mengine, watu hao wamekuwa sawa na sikio la kufa ambalo halisikii dawa.

Wakati umefika sasa wateule hao wa Rais wakabaini kuwa nafasi wanazopewa ni dhamana kubwa na wanapaswa kuzitendea haki kwa kusimamia miongozo na miiko ya uongozi sambamba na kwenda kutatua kero za wananchi. Ni wazi kwamba kama hawatabadilika, Watanzania watashuhudia kila mara Rais anafanya mabadiliko ya viongozi kutokana na aliowateua kutowajibika kama inavyotakiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Madereva wa daladala mnapogoma, hamuikomoi serikali bali wananchi

**USAFIRI** wa Daladala ni usafiri, ambao unatumiwa na rika mbalimbali kutoka sehemu fulani kwenda nyingine.

Kutokana usafiri huo kuwa tegemezi kwa jamii, sasa inatakiwa suala la kugoma kutoa huduma liangaliwe katika tafsiri pana.

Hata kabla ya ndugu zetu wa daladala kugoma kutoa huduma hizo, wanatakiwa kuangalia ni kundi lipi ambalo litaathirika pale wanapogoma kutoa huduma ya usafiri huo.

Usafiri huo sasa unatumiwa na wanafunzi, wafanyabiashara, watumishi kutoka sehemu mbalimbali na jamii.

Kuwapo mgomo kunachangia kwa kiasi kikubwa wanaotumia usafiri huo kutofika kwa wakati katika maeneo wanayoenda, hasa makazini.

Vilevile, kutofika kwa wakati katika maeneo wanayoenda, kunatokana na abiria kukaa vituoni muda mrefu huku wakisubiri usafiri, mara wanapata taarifa kama hizo za mgomo, hakuna usafiri na wanaanza kutafuta njia zingine za kuwafikisha maeneo wanayoenda.

Kinachoshangaza, wenye daladala wanaingia barabarani na daladala zao wanazipaki, badala ya kuchukua abiria, wanacheka tu kila wanakopita vituo vya daladala na kukuta watu wamejaa wakisubiri huduma zao.

Kutokana na kutambulika katika nchi yetu kuwa upo usafiri huo, lakini kuna taratibu zinazofanywa na wamiliki wa vyombo hivyo, baina yao na serikali.

Inajukukana vyombo hivyo vina wawakilishi wao, ambao hata penye changamoto yoyote, wawakilishi huzungumza na serikali, ili kuhakikisha suluhu inapatikana.

Pamoja na changamoto kutokea, madereva wa vyombo hivyo wakaamua kukimbilia uamuzi wa kugoma kutoa huduma ya usafiri, wakidhani kugoma kwao wanaikomesha serikali, kumbe mgomo unawaathiri watumiaji usafiri huo.

Ilikuwa siku ya Jumatatu, Machi 11 wiki hii daladala za Mwanza zikagoma kutoa huduma ya usafiri kuanzia alfajiri kwa madai ya bajaji, zimekuwa nyingi na kuwafanya washindwe kufanya kazi zao vizuri.

Tunajua biashara ni ushindani, hata kama bajaji nazo zinatoa huduma ya kusafirisha abiria, kuna vitu mnatakiwa kukaa meza moja na wenye, bajaji na sio kusitisha huduma.

Ikumbukwe kuwa watu kutoka alfajiri wanatumia daladala kwenda maeneo ya mijini na vijijini, ambako bajaji zinaweza kutofika katika maeneo hayo.

Wapo watu wanatumia daladala kwenda katika vituo vikubwa vya mabadiliko yaendayo mikoani, ambao nauli hulipa ya kawaida. Lakini mnapogoma mnamfanya mtu kukodi bajaji kwa gharama kubwa kwenda kituo cha mabasi ya mikoani.

Wapo wanaopanda daladala kwenda kufuata huduma za afya. Lakini kutokana na kugoma kwenu mnasababisha wananchi kukodisha bajaji kwa bei kubwa kwenda vituo vya afya kupeleka wagonjwa kupata huduma za afya.

Mgomo huo unachangia watu kuingia gharama kubwa kukodi bajaji kwenda maeneo ambayo walitakiwa kufika kwa kutumia usafiri wa daladala.

Bajaji zipo, lakini haziwezi kuchukuwa abiria wengi kwa wakati mmoja na badala yake, watakaowahi wataingia katika bajaji watalipia nauli kama ya daladala na watakapoona hawawezi kukaa vituoni watalazimika kukodi bajaji ili wafike sehemu wanazoenda.

Kutokana na hali hiyo, bajaji na bodaboda ndio zinazopiga debe kubeba wananchi kuwapeleka mijini.

Ieleweke, mgomo unawaathiri wanafunzi wanaolazimika kutembea kwa miguu umbali mrefu, kwani hakuna pikipiki wala bajaji itakayowabeba kwa shilingi 200 za nauli zao.

Hivyo, hii migomo mnayoifanya enyi mnohudumia daladala pasipo kuliangalia hilo kwa mawanda mapana, muelewe hamuiumizi serikali, bali wanaotumia usafiri huo.

HABARI KITAIFA

# CTI yataka ulinzi viwanda vya ndani

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limeiomba serikali na taasisi zake kulinda viwanda vya ndani kwa kununua bidhaa zinazotengenezwa na viwanda ikiwa ni njia ya kulinda hifadhi ya fedha za kigeni.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema hayo jana wakati ujumbe wa shirikisho hilo ulipotembelea kiwanda cha nondo na plastiki cha Lodhia Industries, Kisemvule mkoani Pwani kujionea shughuli za uzalishaji.

Alikipongeza kiwanda hicho kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na kusababisha ajira nyingi kwa watanzania pamoja na kuzalisha bidhaa zenye viwango.

Tenga alisema bidhaa zinazotengenezwa na kiwanda hicho zikiwamo nondo na bidhaa za plastiki ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi kwa kuwa ujenzi wa miundombinu unategemea kuwepo kwa bidhaa hizo.

"Unapojenga barabara, madarasa, madaraja na miundombinu, yote unahitaji chuma kwa kiasi kikubwa sana. Tunajisikia fahari sana kuona mwanachama wetu Lodhia Industries amewekeza kwa kiwango kikubwa kama mnavyoona.

"Lodhia anatekeleza maono ya serikali ya awamu ya sita ambayo siku zote inasisitiza na kuhamasisha uwekezaji kupitia ujenzi wa viwanda vidogo na vikubwa kama hivi vya nondo na plastiki na tunafurahi zaidi kuona mwekezaji huyu ni Mtanzania," alisema.

Aidha, Tenga aliwaomba Watanzania kuwaunga mkono wazalishaji wa ndani kwa kununua bidhaa kwa kuwa zina ubora wa kimataifa na wakati mwingine zinazidi viwango vya baadhi ya bidhaa za nje.

"Bidhaa hizi zina ubora wa hali ya juu na nitafurahi kama Watanzania watachangamkia bidhaa za viwanda vya ndani zikiwamo za nondo na bidhaa kama mabomba ya plastiki kutoka Lodhia Industries ili kuendelea kulinda ajira za watanzania wenzetu ambao wamepata ajira kwenye uwekezaji huu," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Lodhia Industries, Manoj Gopi, aliomba serikali kuweka mkakati kabambe kulinda viwanda vya ndani kama zinavyofanya baadhi ya nchi kwa kuhakikisha zinanunua kwa wingi bidhaa kutoka kwenye viwanda hivyo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kukuza viwanda hivyo na kuongeza nafasi za ajira kwa Watanzania wengi wanaofanya kazi kwenye viwanda hivyo na kulinda hifadhi ya dola ambayo imekuwa ikitumika kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Alisema bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho zimekidhi vigezo vyote vya kimataifa hivyo haoni sababu yoyote kwa serikali kuendelea kuagiza bidhaa za nje kwaajili ya kutekeleza miradi yake ya miundombinu. Aidha, alisema wamekuwa wakiuza nondo kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali ya serikali ukiwamo ujenzi wa daraja la Kigongo Busisi, Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere mkoani Pwani na miradi mingine ya barabara.

"Wenzetu Kenya wameweka sheria kali sana za kulinda viwanda vyao na Uganda wamefanya hivyo hivyo sasa na hapa kwetu kuna umuhimu wa kuendelea kulinda viwanda kwa kuacha kuagiza nje bidhaa kama nondo na bidhaa za plastiki ambazo zinazalishwa hapa nchini na zina viwango vya kimataifa," alisema

Aidha, alisema Lodhia Industries inawekeza dola za Marekani milioni 60 kwenye ujenzi wa kiwanda cha mabati katika eneo hilo ambacho kinatarajiwa kuanza kuzalisha mabati kuanzia mwezi Mei mwaka huu kitakachotoa ajira zaidi ya 500 za moja kwa moja. Alisema kwenye kiwanda cha nondo na bidhaa za plastiki wamewekeza dola za Marekani milioni 45 na kuwezesha ajira zaidi ya 2,000 za moja kwa moja.

# Futi ujazo tril. 57.5 gesi asilia zagundulika

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imesema mpaka Februari, mwaka huu, futi za ujazo za gesi asilia ambazo zimegundulika ni trilioni 57.54.

Imesema kati ya hizo, futi za ujazo trilioni 10.406 zimegundulika maeneo ya nchi kavu na kina kifupi cha bahari na kwamba zilizobaki ambazo ni trilioni 47.13 zimegundulika maeneo ya kina kirefu cha bahari.

Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, alisema hayo juzi jioni wakati wa hafla fupi ya kutia saini hati ya ushirikiano kati ya mamlaka hiyo na Taasisi ya Bahari ya Dar es Salaam (DMI), katika eneo la mafunzo kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia na uanzishwaji wa kituo cha ithibati ya kutoa mafunzo ya usalama na kujihami kwa wanaofanya na wanaotarajia kufanya kazi baharini wakati wa utekelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

Sangweni alisema tayari futi za ujazo za gesi asilia trilioni 10.406 zimeanza kutumika na kwamba zaidi ya asilimia 65 ya umeme unaozalishwa Tanzania unatokana na gesi asilia.

"Na tunaona kwamba gesi iliyopo Tanzania ni nyingi sana na ndio maana serikali iliona iiuze gesi hii kupitia mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia(LNG) ambao kwa sasa serikali iko kwenye mazungumzo na wagunduzi wa gesi hii hasa kutoka bahari kuu,"alisema Sangweni.

Alisema katika kutekeleza mradi huo, pia watachimba visima vya ziada zaidi ya 30 ndani ya bahari kuu.

Kuhusu ushirikiano na DMI, Sangweni alisema kuanzishwa kwa kituo cha mafunzo ya usalama na kujihami nchini, kutawezesha Watanzania wengi kupata mafunzo stahiki, hivyo kuongeza ushiriki wa wananchi wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia zitakazotekelezwa maeneo ya baharini.

Sangweni alisema kwa sasa hapa nchini hakuna kituo chenye ithibati chenye mafunzo ya masuala hayo ya usalama na kujihami.

"Kutokuwapo kwa kituo kinachotoa mafunzo tajwa nchini na hata Afrika Mashariki kwa ujumla wake, kunatulazimu Watanzania wenye ujuzi na uwezo wa kufanya kazi katika miradi inayotekelezwa baharini kwenda nje ya nchi kusomea kozi hizo. Hii ni changamoto kubwa kwa kuwa Watanzania wachache ndio wanaoweza kumudu gharama za kwenda huko nje kusoma kozi husika.

"Kuanzishwa kwa kituo hiki ni hatua ya kuwaandaa Watanzania kushiriki kikamilifu katika mradi wa LNG na miradi mingine ya mkondo wa juu hasa inayotekelezwa baharini. Tayari tumeandika andiko la kuanzisha kituo hicho nchini kwa ushirikiano wa PURA na DMI," alisema. Mkuu wa DMI Dk. Tumaini Gurum, alisema kuanzishwa kwa chuo cha mafunzo ya ithibati kilikuwa kilio cha muda mrefu.


MASTERMIND
TOBACCO TANZANIA LTD

## JOB VACANCIES

### QUALITY CONTROL (QC) INSPECTOR

**Job Summary**

The job holder, reporting to the QC Supervisor / QC Manager, is required to carry out online quality tests in the assigned production line / area and advice the next in line on any areas of improvement to achieve a quality product. In order to realize customer confidence in the quality of the testing, the job holder is required to utilize his/her knowledge, experience, skills and resources at his/her disposal.

**Job Description**

1. Monitor operations to ensure that they meet production standards
2. Inspect, test, or measure materials or products being produced
3. Measure products with Ovens, Balance Weights, CD Express, Pressure Drop, End Testers, Densimeters and other machines as directed by quality Supervisor
4. Select output samples and check them using appropriate methods (measuring dimensions, testing functionality, comparing to specifications etc.)
5. Measure product dimensions, examine functionality and compare the final product to the specifications
6. Accept or reject finished products according to standards
7. Report inspection and test data to Quality Supervisor
8. Perform regular quality assessments on all incoming materials from vendors and outgoing products for deliveries
9. Read blueprints, plans, and specifications to understand the requirements of products and services
10. Recommend improvements to the production process to ensure quality control
11. Document inspection results by completing detailed reports and performance records
12. Educate the production team about quality control concerns to improve product excellence
13. Resolve quality related issues in a timely manner
14. Maintain high confidentiality records of testing, information and various metrics performed by the company
15. Inspect procedures of the entire production cycle to ensure they are efficient and comply with safety standards.
16. Any other assigned tasks by immediate superior.

**Requirements:**

- Basic Education-High school.
- Certification in quality control is preferred.
- A minimum of 2 years' experience in a similar role.
- Computer Literacy
- On Job Training.
- Good math and technical skills.
- Strong understanding of quality control standards and testing techniques.
- Keen attention to details
- Have the knowledge in operating QA lab equipment

### ELECTRONICIAN

**Job Summary**

The Electronician reports to the Technician Supervisor / Production Manager, is in charge of the electrical engineering of the factory and machines. The job holder is required to work with utmost safety, obey all safety rules and regulations, and work efficiently and effectively to complete machining tasks within the stipulated timeframe.

**Job Description**

1) Review blueprints to understand the placement of wiring or to understand the working of the equipment to provide the right service and repairs.
2) Provide suggestions on the lifespan of equipment and other electrical components, advising when certain components should be replaced due to potential risks
3) Ensure all routine maintenance work is handled on a regular schedule to reduce the risk of larger and more complex issues and to reduce costs.
4) Installing electrical systems, components, including control and switchgear cabinets, conduits, wiring, and terminations
5) Study wiring diagrams and manuals to determine correct installation and quality
6) Repair electrical systems, wiring, circuit breakers, equipment and other components so that they remain at full functioning capacity.
7) Test systems with required devices to ensure the system remains safe and that components are compatible.
8) Prevent breakdown of systems by routinely inspecting and replacing old wiring and insulated cables, cleaning circuits etc.
9) Perform effective troubleshooting to identify hazards or malfunctions and repair or substitute damaged units
10) Direct and train workers to install, maintain, or repair electrical wiring or equipment
11) Monitor and adjust production processes or equipment for quality and productivity
12) Set up and operate production machines in accordance with current good manufacturing practices and standard operating procedures
13) Working with QA & QC Controls
14) Any other tasks as assigned by Supervisors

**Requirements:**

- Minimum; Degree in Electrical Engineering or any relevant field.
- A minimum of 2 years' experience in a similar role.
- Electrical Computer Literacy
- On Job Training.
- Good technical skills.
- Strong understanding of quality control standards and testing techniques.
- Keen attention to details

### TOBACCO MACHINE OPERATOR

**Job Summary**

The Operator reports to the services Supervisor / Manager, is in charge of the factory machining and fabrication works. The job holder is required to work with utmost safety, obey all safety rules and regulations, and work efficiently and effectively to complete machining tasks within the stipulated timeframe.

1. Communicate with team members and support teams to ensure continuous production of the correct product at high quality levels with minimal wasted time and materials
2. Operate or monitor multiple pieces of equipment during operation to ensure quality production and minimal unplanned stops
3. Perform necessary pre-operation activities to ensure proper equipment startup and operation on multiple pieces of equipment
4. Ensuring enough raw materials are fed into the machines
5. Conducting periodic checks on output efficiency
6. Gaining a thorough knowledge of a wide range of factory machinery and how it works
7. Conduct quality checks periodically
8. Verify adequate materials and supplies are available to complete operations as needed
9. Troubleshoot problems during machine operation
10. Perform random tests to ensure accuracy
11. Work with others in order to ensure that equipment is in proper working order
12. Shall ensure brand change procedure is followed to avoid brand mix-up
13. Shall work with Quality Assurance (QA) & Quality Control (QC) and take appropriate action on quality related issues
14. Shall identify and reject non-conforming products and inform QA, Technician and Supervisor for the same
15. Shall make sure product is made as per brand specification issued by QA
16. Shall inform Non Tobacco Material (NTM) Supervisor if any wrong NTM is issued on machine or for any shortage of material (NTM)
17. Shall make sure correct tobacco blend is used as per specification and coordinate with Primary Manufacturing Department(PMD) for any shortage
18. Any other task assigned to by the immediate supervisor.

**Requirements.**

- Diploma in mechanical / technical / related field.
- 3-4 years of experience as a machinist in an industrial environment / manufacturing sector.
- Able to work from drawings and sketches and interpret drawings properly to produce the required parts.
- Ability to prepare own working drawings.
- Should possess great attention to details.
- Should possess the knowledge of operating a wide range of metal works machineries
- Knowledge on materials and strength
- Team player and good communicator
- To work with minimum supervision

**NB:**

- All posts, the job location is in Dar es Salaam.
- Deadline is on 5th April 2024.
- All documents (Academic Credentials, Application Letter and CV) shall be in a single PDF file.
- To apply: send via **info@mtt.co.tz**

# Simba tishio kwa binadamu wahamishwa

**Na Ashton Balaigwa**

SIMBA wanne waliokuwa tishio kwa wananchi kutokana na tabia zao za kutoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire iliyoko mkoani Manyara na kuingia katika vijiji vya jirani, hivyo kuhatarisha maisha ya watu wamehamishwa na kupelekwa Pori la Akiba la Rungwa.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imewahamisha simba hao ili kuzuia migogoro kati ya binadamu na wanyama.

Ofisa Uhifadhi wa TAWA, Isaack Chamba, alisema hayo wakati akiwasilisha mada kwenye mafunzo ya siku mbili wanahabari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) yaliyofanyika Bagamoyo mkoani Pwani.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na JET kwa ufadhili wa mradi wa kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa niaba ya serikali ya nchi hiyo. Alisema simba hao waliohamishwa walikuwa wakitoka ndani ya hifadhi na kushinda katika maeneo ya vijiji vilivyo karibu, hivyo kutishia uhai wa watu na mifugo huku wanyama hao nao wakiwa katika hatari ya kuuawa.

"Hawa simba walikuwa wanatoka hifadhini kwenda kushinda vijijini wakivizia mifugo hasa ng'ombe na kuhatarisha maisha ya wakazi wa maeneo hayo. Licha ya jitihada za kuwarudisha hifadhini, waliendelea kurudi katika vijiji hivyo tukaamua kuwahamisha kuwapeleka Pori la Nyasa," alisema.

Kuhusu migongano ya binadamu na wanyama, mhifadhi huyo alisema asilimia 80 inahusisha tembo huku simba, boko, mamba, chui na faru wakichangia asilimia 20.

Ili kupunguza tatizo hilo, alisema TAWA inaendelea kutoa elimu kwa umma namna ya kukabiliana na migongano ya binadamu na wanyamapori.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema mradi wa kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori unatokana na miaka ya hivi karibuni kuwapo kwa changamoto hiyo kwa sababu ya ongezeko la watu, mahitaji ya ardhi kwa ajili ya maliasili, mifugo, kilimo na miundombinu.

Chikomo alisema hali hiyo imesababisha watu na maisha yao kuathiriwa na uharibifu unaofanywa na wanyamapori hasa katika maeneo ya jirani na hifadhi pamoja na shoroba, hivyo kusababisha uharibifu wa mali Pamoja na binadamu kupoteza uhai na kujeruhiwa.

Alisema mradi wa kupunguza migongano hiyo unalenga kuboresha uwezo wa wadau muhimu nchini wanaohusika na udhibiti na utatuzi wa migongano ya binadamu na wanyamapori.

Mradi huo, alisema unatekelezwa na wadau mbalimbali huku walengwa wakiwa wakazi wa vijijini vilivyoko kusini mwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous, katika wilaya za Liwale mkoani Lindi, Namtumbo na Tunduru mkoani Ruvuma.



Daktari wa Macho wa Hospitali ya Polisi Barabara ya Kilwa, Dk. Martin Raphael akimhudumia mmoja wa wananchi waliofika kupata huduma ya upimaji macho bure uliofanywa na Hospitali ya CCBRT kwa kushirikiana na hospitali hiyo na Manispaa ya Ubungo, kwa madereva wa mabasi yaendayo mikoani, katika kituo kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi Luis, Dar es Salaam jana, kuadhimisha Wiki ya Ugonjwa wa Presha ya Macho Duniani. Zaidi ya watu 400 walipatiwa huduma hiyo. Ugonjwa huo, unatajwa na wataalamu wa afya ya macho duniani kuwa wa kwanza kusababisha upofu usiotibika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makinda: Takwimu sensa nyenzo kuhoji masuala yanayohusu jamii

**Na Beatrice Shayo**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Anne Makinda, amesema takwimu za sensa zinawapa nguvu wanahabari kujiamini, kuibua na kuhoji kwa sababu ziko wazi na hakuna atakayewasumbua.

Makinda aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC) kuhusu usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alitoa mfano kuwa katika baadhi ya mikoa, takwimu zilionyesha matumizi ya choo kuwa chini na kipindupindu kilivyoibuka hawakushangaa kwa sababu takwimu zilionyesha, hivyo mwandishi akiandika anaeleza hayo kwa sababu takwimu zipo.

"Huna haja ya kulalamika unanyimwa habari kwa sababu takwimu ziko ndani ya kiganja chako, hivyo wewe ni kuandika kutokana na sensa ya mwaka husika. Hapa kulitakiwa ijengwe hiki mbona hakipo, unafikiri kuna mtu atakufuata kwa sababu unaandika kufuatana na sensa," alisema Makinda.

Alisema lengo la serikali ni kuona matokeo ya sensa yanawafikia wadau wote husani wananchi ili kuyatumia katika shughuli zao binafsi, kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi ikiwamo kufanya uamuzi na kupanga mipango ya kufuatilia na kutathmini shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na serikali na wadau wengine katika maeneo wanakoishi.

Aidha, alisema baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutangaza matokeo ya mwanzo mwaka 2022, ulitolewa mwongozo wa matumizi ya matokeo ya sensa ya mwaka 2022 ni kuongeza uelewa, kufanya uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa serikali.

"Wananchi na wadau wote ili kupanga mipango yao jumuishi kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi, kijamii na kimazingira kutokana na sensa iliyofanyika.

"Katika kuhakikisha lengo hili linatimizwa ndiyo maana serikali ilibainisha kuwa mwongozo huu unakusudia kuyafikia makundi yote ya jamii na ni sehemu ya utekelezaji wa awamu ya tatu na ya mwisho wa utekelezaji wa sensa kama ilivyokuwa katika awamu ya pili na mwanzo," alisema.

Alisema ni dhahiri kuwa sekta ya habari kote duniani imekuwa na mchango wa kipekee katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, utamaduni na pia ni sehemu ya wananchi kuelewa kinachoendelea katika nchi.

Makinda alisema mafunzo haya kwa wanachama yana umuhimu mkubwa kwa kuwa yamevijengea uwezo vyombo vya habari katika kutafsiri, kufanya uchambuzi na namna ya matumizi ya matokeo ya sensa.

# Waonywa kufanya kazi kwa mazoea

**Na Joseph Mwendapole**

WANAWAKE wameshauriwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake wawe wabunifu ili kufanya mambo tofauti na yenye tija kwa jamii.

Ushauri huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, wakati akizungumza na wanawake wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT).

Mkutano huo ulikuwa maalum kwa ajili ya kuwajengea uwezo kuhusu usawa wa kijinsia na uongozi kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika hivi karibuni.

Alisema kuna umuhimu kwa wanawake kufanya kazi kwa bidii na kwa ubunifu kwa kuwa nafasi za uongozi zinategemea ubunifu na kufanya jambo la tafauti katika jamii.

"Nimeona hapa kwenu kuna kiongozi mwenye nafasi kubwa ambaye ni mwanamke. Nafasi hii hakuipata kwa upendeleo bali alifanya kazi kwa bidii na akaonekana. Wengi msibweteke mwigeni mama huyu," alisema.

Liundi alisema wanawake wana uwezo mkubwa katika kuleta mabadiliko kwenye jamii na kitu kinachotakiwa pekee ni kwao kujiamini na kujituma kila wanapopewa nafasi ya kuongoza.

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni "Wekeza kwa Wanawake: Ongeza Kasi ya Maendeleo" ambayo inalenga kuwezesha wanawake kuwa na nguvu ya kiuchumi na kuchukua hatua chanya kufikia juhudi za usawa wa jinsia.

Alisema kwenye semina hiyo wanawake wamepewa elimu kuhusu ujasiriamali, namna ya kuwa kiongozi bora na umuhimu wa usawa wa kijinsia sehemu za kazi lengo likiwa kuwakumbusha wanawake kuhusu nafasi yao katika maendeleo ya jamii na nchini kwa ujumla.

Ramadhani Mungula, kutoka Idara ya Masomo ya Ujasiriamali DIT, aliwataka wanawake wa taasisi hiyo kujikita katika shughuli mbalimbali za kuwainua kiuchumi badala ya kutegemea ajira pekee.

"Ni vizuri kuwa na shughuli nyingine ya kiuchumi itakayokuingizia kipato badala ya kusubiri umestaafu na miaka 60 ndipo unatafuta shughuli ya kufanya. Nakuhakikishia kwa umri huo hutaweza kufanya baishara yoyote ile," alisema.

Pia alisema usawa wa kijinsia katika jamii unategemea fursa, nafasi, majukumu, haki na rasilimali na kwamba ili kila mtu aweze kufikia usawa huu lazima jamii izingatie masuala haya kwa makini ili itasaidia kuondoa migogoro katika jamii.



# Kamati: Hakuna nyongeza ya fedha miradi miwili MoCU

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, imesema haifikiri kuishauri serikali kuongeza fedha yeyote kwenye miradi mikubwa miwili ya ujenzi wa jengo la maktaba pamoja na ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na ofisi katika Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU).

Jengo la maktaba litakuwa na uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500, na ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na ofisi, litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,800.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mussa Sima, aliyasema hayo juzi katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, baada ya ukaguzi wa miradi hiyo.

Alisema hiyo yote ni kwa sababu wana imani fedha iliyokuwa imetengwa naa serikali itatosheleza na miradi itakamilika kwa wakati.

"Tumeridhishwa na maendeleo ya ujenzi huu, lakini maelekezo ya kamati ni haya; menejimenti ya chuo ihakikishe miradi hii inaisha kwa wakati kama ambavyo mkataba ulivyowekwa; na sisi hatuwezi kuishauri serikali kuongeza fedha yeyote, kwa sababu tuna imani fedha iliyokuwa imetengwa itatosheleza na mradi utakamilika kwa wakati.

"Mradi wa kwanza wa maktaba, unaoigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 8.9, umefikia asilimia 75, wakati mradi wa pili wa kumbi za mihadhara na ofisi unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni sita, umefikia asilimia 42.

Zaidi aliongeza: "Jambo kubwa ambalo tunajifunza na leo lengo kubwa la serikali ni kuhakikisha sasa tunaaenda kuimarisha uchumi jumuishi.

Kwa mujibu wa Sima, uchumi hauwezi kukua bila kupeleka wataalam wa kusimamia na kwa sababu jamii ya kitanzania yote imeshaelekea huko, serikali ni lazima ikimbie kuhakikisha inawasaidia kuwapa utaalamu.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, amekagua maendeleo ya ujenzi huo na amegundua ni wa kiwango cha kimataifa.

"Mimi bahati nzuri, ni mtaalam kwenye sekta ya ujenzi. Nimeangalia kwa uchache lakini nimeangalia progress (ujenzi unavyoendelea). Wanaposema leo wako asilimia 75. Kwenye ujenzi asilimia 60 huwa inakuwa ni structural part (muundo), yaani matofali, nondo, nguzo, bims (silabu), ndizo zinazojumuisha asilimiaa 60. Asilimia 40 inakuwa ni upande ule wa finishing (umaliziaji).

"Naomba niihakikishie kamati yako, mkataba wetu wa hii lecture complex (kumbi za mihadhara) ni wa miaka miwili na itakapofika katikati ya mwezi wa saba, tunatarajia jengo hili liwe limekamilika kwa asilimia 100. Hata kama litakuwa halijakamilika kwa asimilia 100, litakuwa tayari kwa kuanza kutumika kutoa huduma." alisema.

Baada ya ukaguzi huo, Makamu Mkuu wa MoCU, Prof. Alfred Sife, aliihakikishia kamati hiyo watahakikisha wanasimamia miradi hiyo kikamilifu na ikamilike kwa wakati.



Watu sita wanaotuhumiwa kwa kosa la kuchoma moto basi la abiria la kampuni ya Saibaba, Februari 27 mwaka huu, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, walipofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga mapema wiki hii, kusomewa mashtaka yanayowakabili. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wabunge watoa siri kiwanda cha vipuri kukosa mwekezaji

**Na Mary Mosha,** HAI

WABUNGE wamesema sababu ya kiwanda cha kutengeneza vipuri cha KMTC kukosa mwekezaji hadi sasa kunatokana na mbinu chafu za wanaoonyesha nia ya kuwekeza, kuja na masharti magumu kushinikiza waruhusiwe kuuza mashine zao, na sio kutengeneza vipuri.

Kiwanda hicho kilichoko chini ya usimamizi wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), kimepangwa kufufuliwa kwa awamu tatu na serikali, kwa gharama ya Sh. bilioni 10.295.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Deodatus Mwanyika, alisema kutokana na mkwamo huo, iko haja kwa serikali kuangalia upya mipango yake ya kukifufua badala ya kuendelea kusubiri wawekezaji.

"Ukiendelea kutafuta mwekezaji hapa utakesha na ukimpata utampata ambaye hana nia njema na kiwanda. Kiwanda hiki ni cha kuzalisha vipuri na mashine kwa ajili ya viwanda vingine. Kwa bahati mbaya yaliyotokea yametokea na viwanda vingi vilikufa baada ya kubinafsishwa.

"KMTC ni moja kati ya viwanda vilivyokufa. Sasa jitihada za kutafuta mwekezaji huko nyuma zikishindikana.

...Naliongea hili kwa sababu nalifahamu. Nilikuwa kwenye Tume ya Umma ya Ubinafsishaji wa Viwanda na hiki kilishindikana kwa sababu, mwekezaji hawezi kuja nchini kwako kuja kutengeneza mashine kwa ajili ya viwanda vingine. Badala yake, wanataka kuuza mashine hapa nchini."

Kabla ya kauli ya Mwanyika, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashantu Kijaji, alisema kiwanda hicho kimeanza kufanya kazi mbalimbali za kuyeyusha vyuma na kutengeneza mashine kwa ajili ya viwanda vingine, licha ya kusimama kwa zaidi ya miaka 40.

Awali, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Amiri Mkalipa, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Hai, aliiomba kamati hiyo kukipigia debe kiwanda hicho ili kitengewe bajeti na kuajiri wafanyakazi wa kada mbalimbali watakaofanya kazi ya kuzalisha mashine nyingi zaidi.

Mmoja wa mafundi wa KMTC, Anna Mosha, alisema wanapokea ofa za watu wote wenye uhitaji wa vipuri pamoja na utengenezaji wa mashine kwa ajili ya viwanda vidogo.

# Serikali kuwashika mkono wanawake kujikwamua kiuchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imesema itaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi, kupitia mikopo ya asilimia 10 ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi na kukuza kipato cha familia.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, aliyasema hayo juzi mkoani hapa wakati wa Siku ya Wanawake Duniani na kueleza kuwa nia ya serikali ni kuona kundi hilo linainuka kiuchumi sawa na wanaume.

"Tunakwenda kuwainua tena wanawake, kwa sababu ya maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba nguvu kubwa sasa tuiishi ile kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Dunuani ya wekeza kwa wanawake, kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii.

Zaidi alisema: "Serikali inatambua mchango wa wanawake katika jamii. Nataka niwahakikishie kuwa serikali itaendelea kuwezesha wanawake kiuchumi, kupitia mikopo ya asilimia kumi na mikopo mingine kupitia mifuko inayowezesha wananchi kiuchumi."

Aprili 13 mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza uamuzi wa serikali wa kusitisha utoaji wa fedha za mikopo kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu, kuanzia Aprili hadi Juni, 2023 ili serikali ijipange kuweka mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hiyo.


Alisitisha mikopo hiyo, wakati akihitimisha hoja zilizotolewa na wabunge wakati wakijadili mwelekeo wa kazi za serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2023/2024.

Katika hatua nyingine, Mongela, amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Aidha alisema Filamu ya The Royal Tour aliyoshiriki Rais Samia Suluhu Hassan, imefungua fursa za kibiashara, ambapo wanawake wameweza kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kujiongezea kipato.

Kuhusu nafasi za uongozi, Mongela, alisema mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, hivyo wanawake wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea.

Mkurugenzi wa Shirika la CWDC, Hindu Mbwegu, alisisitiza wanawake na jamii kwa ujumla, kulinda watoto wa kike wasiolewe katika umri mdogo.





# Shinikizo la damu, kisukari tishio jipya wakazi Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MARADHI ya shinikizo la juu la damu pamoja na kisukari vimetajwa kuwa tishio mkoani Mwanza, baada ya kuwa miongoni mwa magonjwa yanayoongoza kuwa na wagonjwa wengi.

Wagonjwa hao ni wale wenye umri wa miaka mitano na kuendelea, huku chanzo kikitajwa kuwa ni kutokufanya mazoezi pamoja na ulaji usiofaa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza Sekou-Toure, ugonjwa wa shinikizo la juu la damu unashika nafasi ya kwanza kati ya maagonjwa 10 yanayoongoza kwa watu wazima, ukiwa na wagonjwa 5,589 huku kisukari kikishika nafasi ya tano ikiwa na wagonjwa 2,778.

Pia kwa magonjwa 10 yanayoongoza kwa watu wenye umri zaidi ya miaka mitano kutoka kwenye afua zote wagonjwa wa nje, shinikizo la damu linashika nafasi ya nne likiwa na wagonjwa 66,019, huku kisukari kikiwa nafasi ya tisa na wagonjwa 37,670, magonjwa ya maambukizi ya hewa yakiongozwa kwa kuwa na wagonjwa 315,515.

Hali hiyo imemshtusha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu juzi alipofanya ziara na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na UKIMWI katika Hospitali hiyo. Hivyo aliwataka Watanzania kutokupuuzia ushauri wa Mkurugezi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof.Mohamed Janabi na kuhakikisha wanaanza kuchukua hatua.

Alisema kwa miaka mitano iliyopita ilikuwa siyo rahisi kuyakuta magonjwa hayo kati ya 10 hatari na kuitaka jamii kuchukua hatua kudhibiti magonjwa hayo.

Aidha alimuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na timu yake kuhakikisha wanaweka mikakati na mipango mbalimbali ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ili kukabiliana na kasi yake.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy alisema Serikali imenuia kuondoa adha ya matibabu kwa wakazi wa Ukerewe na visiwa vya jirani kwa kutenga Sh. bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wilayani humo.

Akitoa taarifa ya Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza Sekou-Toure, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Bahati Msaki alisema kwa sasa hospitali hiyo inatoa huduma ya kusafisha damu.

Alisema pia Serikali imewasomesha madaktari 17, tabibu za kibingwa lengo likiwa kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.



Ofisa Miradi wa Shirika la Save the Children, Victor Mkiza akitoa mafunzo kwa watumishi wa idara zinazohusika moja kwa moja na mtoto, wakiwamo na Watendaji wa Kata wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga juzi, kuhusu kushirikisha watoto kwenye upangaji wa mipango ya maendeleo ili watoe vipaumbele vyao na kutekelezwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 23 kortini tuhuma kufanya biashara dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS) imewafikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga watuhumiwa 23 wa biashara ya dawa za kulevya.

Watuhumiwa hao wamefikishwa katika mahakama hiyo kujibu tuhuma za kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya bangi, heroin na mirungi.

Akisoma mashauri hayo 18 ya jinai juzi, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Christina Chovenye, wakili wa Serikali, John Hamenya alisema watuhumiwa hao walitenda makosa hayo kwa nyakati tofauti katika kipindi cha Februari na Machi mwaka 2023 katika Wilaya ya Kahama.

Hamenya amewataja watuhumiwa hao ni Juma Lusangija (54), Mwajuma kavula (36), Tayson Marwa (23) Emmanuel Christopher (33), Amos Augustino 34 na Fred Bichuka(37).

Wengine ni Rojasi Daudi (18), Juma Merena (44), Hassan ally Ngwenyau (27) na Gerald Emmanuel (18), Paulo Wilson (25), Joseph Lugenzi, Zamoyoni Andrea (26), Kobelo Ntahondi(42), Raphael Masanja (37), Said kayoka (27), Saidi mselem (22), Haitham Suleiman (31).

Wengine ni Samwel John (31), Joseph lugenzi,(40), Robert Lameck (24), Hillary Nassoro(39), Richard Mushi (30), Izdory Temba (23), Kassim Hamad, (27).

Watuhumiwa wote wamekana mashtaka yanayowakabili na mashauri yao yameahirishwa hadi Machi 14, 15 na 26 mwaka huu kwa hatua ya kutajwa na kusikilizwa baada ya upelelezi kukamilika.

Kaimu Mkuu wa Mashitaka ofisi ya DPP Wilaya ya Kahama, Salome Ngubuni alisema ofisi ya DPP imepokea mafaili kutoka DCEA na wameyafanyia kazi kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mahakamani.

# Mamba wala watu, mifugo wageuka tishio Maswa

**Na Alex Sayi,** SIMIYU

BAADHI ya wananchi wilayani Maswa mkoani Simiyu wamesema ongezeko la mamba katika Mto Simiyu ni tishio kwao.

Wamesema hadi sasa mamba hao wamesababisha madhara mbalimbali ikiwemo vifo kwa watumiaji wa mto huo.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Ipililo, Innocent Kavela alisema hivi karibuni mamba hao wamekuwa wakijeruhi pamoja na kusababisha vifo vya watu na mifugo.

Alisema kumekuwapo na ongezeko la matukio hayo kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

"Haya matukio yemekuwa yakijirudia nakumbuka mwaka jana mamba alijeruhi mtoto nakuuwa mbuzi wawili, lakini kwa mwaka huu mamba amelipotiwa kujeruhi na kusababisha kifo cha mtoto mmoja mwenye miaka tisa aitwaye Masanja Maduhu aliyekuwa anaogelea na watoto wenzake," alisema Kavela.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Bushashi, Mwalimu Meckidad Ruyingo akizungumza na Nipashe alisema wamekuwa wakiwatahadharisha wanafunzi waishio pembezoni mwa mto huo pindi wanapovuka ili kuepukana na matukio hayo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu hatari hiyo, Ofisa Wanyamapori Kitengo cha Ujirani Mwema kutoka Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kanda ya Ziwa, Masinde alithibitisha kutokea kwa madhara hayo na kutoa tahadhari ya uwepo wa ongezeko la wanyama hao linalosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Masinde alisema matukio ya mamba kujeruhi na kuuwa watu hivi sasa yanatokana na mtawanyiko wa maji kwenye maeneo mengi ikiwemo Mto Simiyu, hali inayosababisha mamba hao kuongezeka kwenye vijito vinavyolisha mto huo.

"Wananchi wanapaswa kuchukua tahadhali kwa kuwa mamba wameongezeka na wanawafuata samaki aina ya kambale ambao ni chakula chao. Lakini kwa kuwa mamba ni mnyama anaekula myama hivyo anaweza kuhatarisha maisha ya watu na mifugo pia,"alisema Masinde.

Hivyo aliwataka wananchi kuzijua sifa za mnyama huyo na hatari zake ili waweze kuondokana na imani potofu dhidi yake kwa kuamini kuwa hutumwa na watu kusababisha uharibifu na vifo.

Alisema: "Kwanza ni vema wazazi wasiwaache watoto kwenda kucheza mtoni au kunywesha mifugo peke yao maana mamba ana sifa ya uhimilivu wakati wa mawindo, hukaa eneo moja kwa zaidi ya saa nane, anauwezo wa kukimbia mwendo wa kilometa 34 majini, huzamisha mwili na kubakiza macho na pua, ana meno kati ya 28 hadi 64 hivyo ni mnyama hatari sana".



Ukurasa 14

UTALII VS MASLAHI UMMA...
Serikali yatanua wigo wake kudhibiti wanyama wasiingie shambani, makazi




**Inapendeza, wananchi waachwe wachague viongozi wao waliko**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA MACHI 15, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Samia Miaka Mitatu, inavyoambatana na umri wa mradi mbolea unaomlipa

**Na Mwandishi Wetu**

UTASHI wa kisiasa uliojenga mazingira wezeshi, kitaalamu, ni nyenzo muhimu inayosaidia kasi ya ukuaji tasnia ya mbolea nchini. Hapo inatajwa, kipindi cha miaka mitatu, uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ni sauti yake Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Joel Laurent, anayeema katika msimu wa kilimo wa 2022/2023, Rais Dk. Samia na serikali yake, walikuja na mpango kabambe kitaifa, wa kutoa ruzuku ya mbolea kuimarisha sekta kilimo, itoe mchango mkubwa katika uchumi wa taifa.

Anasema, mpango huo sasa unaleta hamasa kubwa kwa wakulima, ukiongeza uzalishaji mazao, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na chombo anachosimamia.

Mkurugenzi huyo anasema, katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi huo, Tanzania imeshuhudia kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea na visaidizi vyake, kutoka 12 hadi 15, hivyo kuchochea ongezeko la upatikanaji mbolea nchini.

### ONGEZEKO LA BAJETI

Vilevile anasema, miaka mitatu ya uongozi wa, Rais Samia kutimia sasa, bajeti ya Wizara ya Kilimo imepanda kutoka shilingi 751.123,280,000 za mwaka 2022/2023 hadi shilingi 970,785,619,000 za sasa, mwaka 2023/2024.

Laurent anaitafsiri kuwa bajeti yenye msukumo mkubwa kiserikali, katika kuimarisha sekta ya kilimo inayoajiri asilimia 75 ya Watanzania, hasa vijijini.



Wauzaji wa mbolea Penina Mwita (kulia mwenye fulana ya rangi inayofanaa na nyekundu) na Leonald Mpayo (wa pili kulia), wakimuhudumia mteja aliyefika kwenye Banda la Maonyesho ya Kilimo, mkoani Mbeya mwaka juzi. **PICHA: MTANDAO.**

Mkurugenzi huyo wa TFRA, anayataja mafanikio yanasukumwa pia na ujenzi wa maabara ya kisasa inayochambua mbolea, mkoani Dar es Salaam, hapo akiitafsri ni jitihada za makusudi serikalini kutatua changamoto kwenye eneo la mbolea na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

Hapo anasaudiwa na ufafanuzi wa mtaalamu, Louis Kasera, Kaimu Mkurugenzi Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja wa TFRA, anayeieleza kuwa uwekezaji serikalini na kuundwa mazingira wezeshi kiuchumi, mahsusi katika mbolea.

Zao lake linaloitwa na wachumi 'multiplier effect' (jambo moja kusukuma kuongezeka lingine), sasa inavutia ongezeko la wawekezaji wa nje kuchangamkia fursa zilizoko katika tasnia ya mbolea.

Kasera anabainisha moja ya kichocheo kikubwa ni upatikanaji malighafi za viwanda ya kuzalisha mbolea, hapo akiorodhesha mifano ya madini ya fosfeti, gesi asilia tani za ujazo trilioni 57, kuwapo makaa ya mawe ya kutosha, madini ya chokaa na madini mengine yanayohitajika.

Katika nafasi ya pekee, Kasera anamtaja Rais Samia na safu yake viongozi waandamizi katka Wizara ya Kilimo, wakiwa chachu ya uwekezaji katika kilimo, nyuma yake kukiwapo fursa pana za viwanda vya mbolea.

Hapo, Kasera anatoa ufafanuzi kwamba Tanzania ni taifa lililozungukwa na soko kubwa la nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, lenye idadi ya watu zaidi milioni 600 wahitaji wa bidhaa zinazohusiana na shambani.

### HALI YA UZALISHAJI

Kuhusu kiwango cha uzalishaji, TFRA inasema asilimia 90 ya mbolea zinazotumika nchini, aagizwa kutoka nje na asilimia 10 zilizobaki zinazalishwa na viwanda 15 vya nchini, kwa mujibu wa takwimu za TFRA.

Hadi sasa, azma ya serikali ni kuona Tanzania inajenga mazingira ya kujitosheleza kwa pembejeo kama mbolea, ili kuepuka uagizaji nje, ikikwepa gharama za matumizi ya fedha za kigeni.

Kimsingi, kiwanda cha Minjingu kilichopo mkoani Manyara, ndicho kikubwa zaidi kikizalisha asilimia 80 ya visaidizi vya mbolea.

Viwanda vingine vinavyozalisha visaidizi ni; ABM Equipment kilichopo Tanga na Dodoma Cement cha jijini Dodoma.

Pia kuna; Kahela Traders, Keen Feeders Co. Limited, Sianga Agro Trade Company, Mtali Agrotraders na Amka Feeder's, vyote vinatengeneza mbolea za maji.

### FURSA ZA UWEKEZAJI

Serikali ya Awamu ya Sita na kwa utashi wa kisiasa wa Rais Dk.Samia, amebeba jukumu la kuwavuta wawekezaji nchini wa viwanda vya mbolea.

Hapo kunatajwa kuwapo fursa za uwekezaji kwenye mbolea, ikigusa mazingira wezeshi, masoko ya ndani na nje, huku nyuma yao wakisimamiwa na nguzo ya kisera kutetea nyendo zao kutoka katika mamlaka za kisiasa kitaifa, hata kusaidia ng'ambo ya pili penye; Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu.

Tanzania inajivunia eneo lake kijiografia, kukiwapo soko kubwa

Inaendelea Uk 12

## UCHUMI

WATAALAMU NA HOJA MBOGA INALIPA...

# Wadau kilimo watumia Siku Wanawake kuhamisha 'dada' waliokwama bustanini

**Na Renatha Msungu ARUSHA**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake hivi karibuni, Kituo cha Kilimo cha Mboga, World Vegetable Centre, jijini hapa ikatumia fursa hiyo kuwainua kiuchumi wanawake wa kituo cha Faraja, ikiwapa miche ya mazao ya mboga, kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Inatajwa kuwa dhamira hapo ni kuwakwamua kinamama hao, ambao wametelekezwa na wengine kuzalishwa na kuachiwa kutunza watoto.

Ikaelezwa, ni namna ya kuwazibia pengo hilo la kiuchumi kuhakikisha kila mwanamke anainuka katika namna zote kupitia taasisi World Vegetable Centre, dira ni kuona wanaanzisha bustani za mboga na kuwatengenezea kipato.

Wanufaika waligaiwa miche hiyo wanatoka vituo viwili vilivyopo Arusha, ambako kuna kinamama na kinadada waliopewa mtaji wa kuanzisha bustani za kujikimu kimaisha.

Nipashe iliyokuwapo katika hafla hiyo, ilishuhudia miche ya matunda, pia mbegu za mboga za majani walizopewa kinamama wanaojishughulisha kiuchumi na kukimu maisha yao.

Meneja Msaidizi wa Rasilimaliwatu wa World Vegatables, El Frida Munuo, anaanza kwa kwa kuwatamka wanawake kuwa 'jeshi kubwa', hivyo hawapaswi kuogopa kitu chochote, badala yake wanapaswa kufanya kazi kwa bidi kujikwamua kiuchumi ilivyo, kwa wanawake wengine.

Anasema, World Vegetable Centre, Elfrida anasema imeamua kutoa miche hiyo, iliyo bora kwa ajili ya mkulima wa mazao ya bustani, rai yake akihimzia wanufaika ambao wengi ni wasichana akiwataka kujikita katika kilio cha bustani, kwani ni rahisi kukiendesha na kinamkwamua mtu kiuchumi kirahisi.

Hapo akataja mkakati wa taasisi yao watakuwa wanawatembelea wanufaika tajwa, ili kuhakikisha wanaendesha kilimo cha mboga chenye tija, kinachoweza kuwainua kiuchumi vijana hao wa kike katika maisha yao kila siku,

ElFrida huku akikitetea kilimo 'kinalipa' ndio maana vijana wengi hivi sasa wanakichagamkia kujikita, hasa katika mazao ya bustani, ambayo hukua na kuzaa kwa haraka na kuwaletea faida wakulima wa mazao hayo.

Meneja Rasilimaliwatu wa World Vegetable Centre Upendo Laiser, anasema tayari walishatembelea vituo hivyo viwili, walikopata uhakika namna wanufaika wao wasichana watafanya vizuri kupitia msaa wa miche waliopewa.


Wanawake wa kituo cha World Vegetable Centre, walipotembelea kituo cha kinamama cha Faraja na kuwapa msaada wa mbegu. **PICHA; RENATHA MSUNGU.**

Kwa mujibu wa Meneja Upendo, miche hiyo waliokabidhiwa kwa ajili ya kujiinua kuichumi na kituo kinachotoa msaada, kinahakikisha tajwa havibaki nyuma kwenye kilimo cha mboga, ambacho sasa ndicho kinawatoa wakulima wengi.

Anawasistiza wakulima wanawake wasibaki nyuma kwenye kilimo, kwa sababu ndicho kinasaidia kuamua mengi, ikiwamo kujiinua kiuchumi ndani ya familia.

Kwa mujibu wa Upendo, kituo hiko kiliadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu, kwa kuwatembelea wanawake mbalimbali wenye changamoto za kimaisha na ikawapa miche ya mboga wahitaji, kwenda kupanda iwaanzishie maisha mapya ya kilimo bustanini.

"Wanawake amkeni, 'kilimo kinalipa' hususani kilimo cha mboga na matunda huwatoa kimaisha. Watu wengi sana hapa nchini, ambao wanafuata kanuni

bora za kilimo wanafanikiwa," anasema Upendo.

### WAKULIMA WANAVYOSEMA

Kauli ya jumla, wanakishukuru kituo cha World Vegetable Centre, kwa kuwasaidia wakulima wengi wa Arusha ndani na nje ya jiji hilo, ikiwapatia mafunzo pamoja na mbegu za kupanda katika bustani zao kwenye maeneo hayo.

Saada Hussein, mkulima kutoka Dodoma anasema amenufaika na kituo hicho cha mboga akipata mbegu bora zinazomsaidia yeye na familia kujiendesha kimaisha, kwa kufanya biashara ya mboga.

Anaiasa jamii, inapaswa kuamka na kujikita katika kilimo bora, kinachomuinua kiuchumi mkulima yeyote, endapo mkulima atafuata masharti vilivyo na kupangiwa na wataalam wa kilimo namna stahiki ya kutekeleza kazi yake.

Mwingine, Matrida Jared, anakisifu kilimo cha mboga kinalipa sana, hivyo wamekuwa wakiwashauri wakulima walime mazao kama ya nyanya, pilipili hoho na bidhaa nyingine

zinazokua haraka na kutoa faida kwa wakulima.

Matrida anashauri wakulima wenzake wa jijini Arusha, wanapaswa kutumia fursa zinazotolewa na kituo hicho kilichowasaidia, waweze kujikwamua kiuchumi katika mambo mbalimbali ambayo wanafanya.

Anasema ni kituo kinachohifadhili mbegu, pia hutoa elimu kwa wakulima wanaotembelea mahali hapo, lengo ni kutaka waende kufanya kilimo cha mboga chenye tija kwa jamii wanachofundishwa.

### MTAFITI& MKURUGENZI KITUO

Mary Matovolwa, ni Mtafiti Msaidizi, anayesema wao hufanyia utafiti mbegu na baadaye wanazipeleka katika kampuni husika za mbegu kwa ajili ya kuanza kuzisambaza kwa wakulima hapa nchini.

Anasema wameshafanyia utafiti mbegu nyingi baada ya kuziona zinafaa, wakazipeleka sehemu husika kufanyiwa kazi na baadae wakulima wanapatiwa, kwa ajili ya kuendesha kilimo chao cha kila siku.

Mtafiti huyo anafafanua kuwa, wanafanya hivyo kuhakikisha wakulima wa mazao ya bustani wanapata kilicho bora kutoka World Vegetable Centre.

Kutokana na hilo, sasa anatoa wito wa kitaalamu kwa jamii kuacha kubweteka na wajikite katika kilimo cha mazao ya bustani, ambacho kitawainua kiuchumi wao na familia zao

Dk. Gabriel Rugalema ni Mkurugenzi wa kituo hicho cha World Vegetable Centre, anayefafanua kituo hicho sasa ni kikubwa na kinafanya kazi na upeo wa mataifa mbalimbali, kutokana na umuhimu wa kilimo wanaoutoa.

Anasema wamekuwa wakifundisha watu mbalimbali, wakiwamo wanafunzi kutoka vyuoni kufanya mazoezi kwenye kituo hiko kwa ajili ya kupata ujuzi wa kilimo.

Dk. Rugalema anasema, moja ya mikakati wamejiwekea kituoni ni kuhakikisha wanawainua wakulima hapa nchini katika kilimo cha mazao ya bustani ambacho watu wanafanya.

Pia, anaishukuru serikali hususani Wizara ya Kilimo, kutokana na ushirikiano mkubwa wanaoupata kuhakikisha kituo hiko kinasonga mbele katika shughuli zake za uendeshaji wa kilimo cha mboga pamoja na kuhifadhi mbegu mbalimbali za mazao ya bustani.

## SAMIA MIAKA MITATU, INAVYOAMBATANA NA UMRI WA MRADI MBOLEA UNAOMLIPA MKULIMA

Inatoka Uk 11

la mbolea kwenye nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

MIUNDOMBINU/USALAMA CHAKULA

TFRA ina ufafanuzi wa mtaji wa soko katika ujenzi wa miundombinu ya kisasa, barabara na reli zinazoimarisha sekta ya uchukuzi.

Inataja wastani asilimia 70 na zaidi ya Tanzania inapitika sasa kwa barabara za lami, huku ujenzi wa reli ya kisasa ukiendelea, kuanzia jiji la biashara Dar es Salaam, kwenda nchi jirani za Afrika Mashariki kama vile Rwanda na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC).

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa TFRA, Happiness Mbelle, anasema uamuzi wa serikali kuweka msukumo mkubwa katika tasnia ya mbolea, ina mchango mkubwa katika kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Hiyo anaitaja inaanzia katika matazamo wa ongezeko kubwa la watu, asilimia 4.8 kila mwaka (sasa Tanzania ina watu milioni 63, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, 2022), inayoendana na malighafi viwandani.

Anafafanua, katika miaka mitatu ya uongozi wake, Rais Samia, amekuwa akiwahimiza watendaji wa ngazi zote, kusimamia kikamilifu katika sekta ya kilimo itoe mchango katika uchumi wa taifa.

Mbelle anafafanua kuwa, Rais amekuwa akisisitiza kwamba uamuzi ya serikali kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, unalenga kuwawezesha kutumia fursa hiyo kuzalisha kibiashara, wakijitosheleza kwa chakula na ziada ya kuuzwa nje ya nchi kuingiza fedha za kigeni.

### MFUKO PEMBEJEO

TFRA inakumbusha msisitizo wa Rais Dk. Samia wakati wote ni katika 'kuongeza uzalishaji shambani', kwamba ni nyenzo itakayoifanya serikali kuanzisha Mfuko wa Pembejeo, utakaotumika kwa dharura, hasa pale bei zake zikapotikisika kilimo.

Mipango mahsusi ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa mbolea nchini inajumuisha kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha Itracom Fertilizer Limited jijini Dodoma na upanuzi wa kiwanda cha Minjingu mkoani Manyara, ikiaminika vyote vitawapunguzia adha wakulima wa kununua mbolea kwa bei kubwa.

Meneja wa Uhusiano, Mawasiliano na Elimu wa TFRA Matilda Kasanga, anasema uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea nchini unaendelea, ukihusisha wadau kuanzia na wizara mama ya Kilimo.

Maeneo mengime anayataja kuwa, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, waingizaji na wazalishaji wa mbolea na mawakala wa mbolea, ili kuhakikisha kwamba elimu ya matumizi ya mbolea katoka kilimo haikwami kokote.

Hapo anataja lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa wakulima wengi nchini wanaelimika, ili waweze kuongeza uzalishaji shambani.

### HARAKATI ZA BASHE

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, hadi sasa anasimama kuwa mhimili mkubwa wa wa kilimo nchini, kutoka nguzo ya wizarani, katika maeneo kama; sera za kilimo, usalama wa chakula, umwagiliaji na ushiriki wa mkulima, kusimamia matumizi bora ya ardhi ya kilimo; mafunzo na huduma za ugani; pia kusimamia maendeleo ya zana za kilimo na pembejeo, ikiwamo mbolea.

Hadi sasa, Wizara ya Kilimo ina dira ya kuwa "kiini cha kutoa mwongozo wa sera na huduma kwa kilimo cha kisasa chenye tija, faida na ushindani kibiashara ili kuimarisha ustawi wa wananchi, usalama wa chakula na lishe ifikapo mwaka 2025."

Katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, kitakwimu kumeshuhudiwa ongezeko la matumizi ya mbolea shambani, kutoka wastani wastaniwa tani 475, 000 mwaka 2020/2021 hadi ku tani 848,000 kwa mwaka 2023/2024.

Hiyo inatoa tafsiri kwamba, wakulima wanabadilika kwenye kilimo cha kisasa, maisha yao kiuchumi, uzalishai kitaifa uliongezeka na hali ya taifa kujitosheleza kwa chakula na kuwapo ziada ya kuuza.

### WASOMI WAKIMBILIA KILIMO

Pia, kuna nyendo za mageuzi kihistoria tangu uhuru, safari zaidi ya nusu karne, wasomi waliokiona kilimo kama 'adhabu au mateso kwao', sasa wageuka wadau wake.

Rais Dk. Samia akiweka historia, pale vijana wengi wasomi wameanza kukimbilia kilimo kama chanzo cha 'asali na maziwa' ikiwaepusha kutoka ulingo wa kukosa ajira, nao wakionekana katika kundi la wakulima hodari wa mazao mbalimbali ya biashara na chakula.

Mfano hai, unajitokeza katika Mradi wa Jenga Kesho Bora (BBT), ulioanzishwa na Rais akiwa na kundi la vijana 812, 212 wakiwapo katika shamba la Chinangali mkoani Dodoma.

Mpango huo unalaenga kuwapa vijana ajira ya uhakika, wakijipatia mashamba ya kujiendeleza, Serikali ya Awamu ya Sita iliyoposimama nao kuwaelimisha siri 'kilimo kinalipa' na iko 'iko jirani na utajiri.'

Pia, hamasa ya Rais Samia kujenga viwanda vya mbolea, leo imezaa matokeo chanya ya kupatikana mbolea zenye bei nafuu, hivyo kuongeza uzalishaji, usalama wa chakula, kudhibiti mfumuko wa bei za vyakula na kuinua kipato cha mkulima mmoja mmoja, ikitoa majibu 'miaka mitatu ya Dk. Samia imemuinua mkulima.'

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Inapendeza, wananchi waachwe wachague viongozi wao waliko






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

ZAMANI tukisoma shule za msingi, mwalimu aliyeonekana kufanya vizuri katika kazi yake ya ufundishaji, hususan katika shule za umma ambazo zilikuwa nyingi, alihamishwa.

Mwalimu huyo alihamishwa, ama kwa kupandishwa cheo na kuwa Mratibu

wa Elimu wa Kata au Tarafa au wakati mwingine kupelekwa shule nyingine ili kuboresha elimu na wengine kuwa wakaguzi wa elimu.

Hatua hizo zilihuzunisha wanafunzi, kwani walikuwa wakiondolewa walimu

waliowapenda kutokana na ufundishaji wao uliozaa ufaulu na kuipa shule sifa kubwa.

Vivyo hivyo, ilikuwa kwa walimu wenzao waliotarajia kuchota hekima na weledi wa ufundishaji kutoka kwa wenzao hao waliohamishwa na kupandishwa vyeo kwa manufaa ya Taifa kielimu.

Baadhi yao kutokana na uchapaji kazi wao, walijikuta wakipata madaraka makubwa katika Wizara ya Elimu, ambako walichangia uzoefu wao katika ufundishaji na kuijua barabara sekta hiyo muhimu kwa jamii.

Wakati huo aliyeharibu kazi, tulikutana naye mitaani akijishughulisha na biashara zingine zikiwamo za kuuza kahawa na karanga au kashata, kwani hakuzingatia kilichomweka shuleni kufundisha watoto.

Siku hizi mambo yanakwenda yakibadilika, anayeharibu sehemu moja, huwezi kushangaa kwamba hachanganyikiwi, kwani kuna eneo lingine anaamini anaweza kuangukia katika kuwajibika, ili mradi ameshaingia kwenye mfumo.

Hatukatai, kuna wakati mwingine watu hutumbuliwa kwa sababu ya majungu na uchunguzi unapofanyika na kubaini kuwa ni majungu, wamekuwa wakirejeshwa kazini na kufanya majukumu yao kama inavyotakiwa bila matatizo.

Lakini wapo ambao hubainika kufanya matatizo, lakini hukaa pembeni muda mfupi na kurejea ngalawani na kuendelea na safari

Pia, zamani tulisikia sana mtu anapatwa na kesi, anasimamishwa kazi kupisha uchunguzi na kumalizika kesi, kama alionekana hana hatia alirejea kazini na kulipwa haki zake.

Nakumbuka mwaka 1995, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kwenye mkutano na wanahabari, alisema kuwa enzi zao kama kiongozi

alihusishwa na tuhuma hata kabla hajathibitika, aliwekwa pembeni.

Alitoa mfano uliotokea hata Uingereza, ambako Waziri mmoja 'alipita' na 'dada wa barabarani', alichokifanya Waziri Mkuu wakati huo, hata

kabla haijathibitishwa, aliteua Waziri mwingine kuziba nafasi yake.

Lengo la mifano hii ilikuwa ni kulinda heshima ya uongozi wa mteuzi na mteule. Najua mambo haya hayafanywi na mteuzi, bali wasaidizi wake wenye jukumu la kumpelekea majina yaliyofanyiwa uchunguzi na tathmini ya kutosha, ingawa wakati mwingine inaonekana hapati usahihi, kutokana na maslahi ya baadhi ya walio karibu nao.

Nakumbuka pia kuna wakati Rais wa Awamu ya Tano, Dk John Magufuli, akizungumzia mmoja wa wateule wake, alisema alipotaka kumteua, wasaidizi wake walimfuata na kumwambia hafai hata kidogo.

Lakini kumbe walikuwa na sababu zao, kwani aliwapuuza na baadaye alimteua na kuonekana mchapakazi wa mfano kuliko wenzake.

Labda pengine jambo la kufanya ni kwamba mtazamo wangu unaangukia, Watanzania ni wengi na mteuzi hawezi kumjua mmoja mmoja kwa tabia na hulka yake na ndiyo sababu mabadiliko tunayaona zaidi kwa wakuu wa mikoa na wilaya hao hao. Nadhani mfumo ubadilike.

Inapendeza, wananchi waachwe wachague viongozi wao wilayani na mikoani na kumwachia Rais awaapishe kwa niaba yao na wakiharibu wawe na mamlaka ya kuwatumbua muda wowote?

Hilo linawezekana ili kuondokana na kuhuisha watu kama chuma chakavu. Mungu endelea kutumulika!

UCHUMI

## UTALII VS MASLAHI UMMA...

# Serikali yatanua wigo wake kudhibiti wanyama wasiingie shambani, makazi

**Na Jenifer Gilla**

UTALII wa wanyamapori, hadi sasa ndio inayoongoza kuliingizia Taifa mapato ya fedha za kigeni. Kwa mujibu wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023, sekta ya utalii ilichangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 21 ya pato la taifa.

Vilevile, katika utalii wa wanyamapori nao unatajwa kuchangia takribani asilimia 17 ya pato la taifa, huku ikitoa ajira milioni 1.5.

Licha ya mchango mkubwa katika pato la taifa, utalii wa wanyamapori unakabiliwa na changamoto kubwa, ikiwamo migogoro na binadamu, hata kuchangia shida katika kivutio hicho.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), inataja eneo mojawapo lenye migongano, ni athari za mabadiliko ya tabianchi, ni ukame unaosababisha wanyamapori kuvamia makazi ya binadamu, kutafuta maji na chakula. Hadi sasa hali hiyo inashuhudiwa huko Nachingwea, mkoani Lindi.

Pia, binadamu wanatajwa tishio kwa wanyamapori kutokana na kutumia njia isiyo rafiki kuwazuia, pale wanapokaribia makazi yao, hasa wanapowaua au kuwajeruhi.

Hilo limeifanya Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzisha Makakati wa Kitaifa wa Kusimamia Migongano kati ya Binadamu na Wanyamapori kwa mwaka 2020 hadi - 2024, ikielekeza taasisi zote za hifadhi kufuata mwongozo huo kutatua changamoto zinazojitokeza.

TAWA na wadau wa maendeleo ya uhifadhi kama Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), wamekuwa wakifuata mwongozo huo, wakishirikiana na serikali kutatua migogoro tajwa, ili wanyama waishi na binadamu kwa amani.

Mnamo tarehe 23 mwezi uliopita, wadau wa uhifadhi chini ya uratibu wa Chama cha Waandishi wa habari za Mazingira Tanzania (JET), walikutana na wanabari katika mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu migogoro hiyo, wakiwaeleza namna wanavyokabiliana na shida hiyo.

Ni mafunzo yanayobeba maudhui ya kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori nchini, yanayotekelezwa na GIZ, kwa niaba ya serikali ya Ujerumani.

Mradi unanuia kuhakikisha binadamu na wanyamapori wanaishi kwa amani, wakitumia kwa pamoja rasilimali zinazowazunguka kwa namna enedelevu, ukiwaboreshea uwezo wadau muhimu nchini wanaohusika kudhibiti na kutatua migogoro hiyo.



Eneo la shamba lililovamiwa na tembo. **PICHA: MTANDAO**

Mshauri wa mradi huo, Anna Kimambo, anasema walengwa wakuu ni wakazi wa vijijini vilivyoko Kusini mwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous, katika wilaya za Liwale (mkoa wa Lindi), Namtumbo na Tunduru (mkoa wa Ruvuma).

Hata hivyo, wilaya jirani ya Nachingwea mkoani Lindi, hadi sasa nao unakabiliwa na tatizo la vijiji vyake kukabiliwa na shida ya uvamizi wa tembo.

Mtaalamu Anna, anasema katika mradi huo wanatafiti katika ngazi za jamii kutambua athari kwa kaya tofauti, masuala ya kijinsia, mikakati ya kukabiliana na hali hiyo, na ufanisi wa mbinu za kupunguza migongano na wanyamapori.

Anasema, pia wanaandaa mkakati wa kanda ukiwa mwitikio wa haraka unaoshirikisha wadau wote husika kuwezesha mafunzo ya mbinu mbalimbali za kupunguza madhara, kwa jamii zilizoathirika zaidi.

Pia, wanabuni na kuimarisha miradi ngazi ya jamii, kufanya tathmini ya awali ya madhara na mtawanyiko wa wanyama waharibifu katika ukanda wa Ruvuma na ushoroba wa Selous-Niassa.

Mtaalamu huyo anasema wanaendeleza mafunzo ya haki za binadamu na kanuni za utawala wa sheria zinazolengwa kwa vikosi vinavyoitikia haraka kwa taasisi husika.

Anasema namna watakavyotumia uzoefu kimataifa kwamba: "Tunawezesha mashauriano ya kuweka mfumo wa kimkakati wa kuitikia haraka matukio ya wanyama waharibifu na kutoa huduma za ushauri kuhusu suluhisho la muda mrefu kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori."

Eneo lingine analolitaja ni kujengea uwezo wizara na idara ya wayamapori, kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori na huduma za ushauri, kuhusu taratibu za uendeshaji, pia kanuni na itifaki.

**MZIZI WA VITA**

Ofisa Uhifadhi Kitengo cha Operesheni na Udhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu (TAWA) Izaack Chamba, anasema chanzo cha mgogoro ilianza kushika kasi mwaka 2018.

Anasema mwenendo wa matukio ya migongano, umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa asilimia 23.76 na uharibifu mkubwa ukiwa kwenye mazao, akitaja tembo wanaongoza uharibifu huo kwa asilimia 80.

Pia, anasema ukubwa wa tatizo uko katika wilaya 44 zilizothirika na migogoro, kati yake 10 zinazoongoza zinajumuishwa na: Busega, Kilwa, Meatu, Nachingwea, Rufiji, Lindi, Manyoni, Tunduru, Bunda na Itilima.

Anasema kwa sasa, TAWA inatumia mwongozo huo kuelimisha jamii, pia mafunzo askari wanyamapori vijijini na mbinu rafiki za kukabiliana na wanyama, mfano kulima pilipili, kuweka kengele na senyenge katika mipaka ya shamba,

Pia, wamekuwa wakipeleka vijana wazawa kwenye maeneo yenye migongano shule kujifunza mbinu hizo za ukabiliana na wanyamapori hatari kwao.

Anataja mwaka juzi, walitoa mafunzo kwa vijana 20 wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, huku wengine 17 walitoka mikoa ya Mara na Simiyu.

"Desemba mwaka jana walipeleka vijana 120 wanaotoka kwenye vijiji vilivyopo kwenye shoroba za wanyamapori, katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, ili kupata mafunzo ya njia rafiki za kukabiliana na wanyamapori," anaeleza

Anataja hatua nyingine ni kufanyika doria za kila mara vijijini kudhibiti wanyama wakali na waharibifu. Chamba anasema wanawahamisha wanyama kutoka hifadhi moja hadi nyingine, pale wanapoleta madhara katika eneo la mwanzo.

Pia, anasema TAWA inajenga vituo vya askari wanyamapori katika vijiji vyenye mwingiliano wa binadamu, ili kuongeza nguvu ya kukabiliana na migongano na mwaka 2021/22 walijenga vituo 16 katika wilaya; zikiwamo Tunduru- Chingulungulu, Nzega-Ndala.

Chamba anasema, chombo kinanunua vitendea kazi vya askari wanyamapori, kurahisisha utendaji kazi wao na mwaka 2022/23, walinunua pikipiki 50 na magari sita.

Lingine linaloendana nazo ni matumizi ya teknolojia ya kisasa kukabiliana na wanyamapori, ikiwamo helikopta na kuwafunga wanyama vifaa maalum kufahamu maeneo walioko.

Mkuu wa Mawasiliano Wizara ya Maliasili na Utalii, John Mapepele, anasema serikali imebuni miradi hiyo, kupunguza migongano ya binadamu na wanyamapori, kushirikiana na wadau wa uhifadhim, wakiangukia kutoa elimu hiyo kwa jamii.

Hapo anataja kwa upekee, juhudi zake Rais Dk. Samia, anayeshirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira kufanikisha hilo nchinim huku akifafanua kwamba wizara hiyo sasa iko katika falsafa za 'Uhifadhi na Utangazaji Utalii', inayovuta mafunzo stahiki kwa waandishi wa habari, wawe sehemu ya mipango kuimarisha uhifadhi kupitia utangazaji.

Mapepele anakumbusha uhusiano ulioko, wanatoa uhifadhi, pia kutunza maeneo ya hifadhi, ili kusaidia kuepusha migongano kati yao na wanyama.

Mtaalamu wa nadharia ya 'Migongano ya Binadamu na Wanyamapori', John Noronha, anaeleza suala la kuzuia migongano linahitaji kuwapo suluhisho tofauti, kulingana na aina ya eneo, hivyo kutambua maisha ya eneo tajwa, kabla ya kupeleka suluhisho.

"Suluhisho ya Selous (hifadhi) ni tofauti na kuchinja tembo wa Selous. Ni wakali, kwa sababu wanawindwa" anasema.

Hapo ana ufafanuzi kwamba, kuwapo taarifa hafifu zinazohitajika wanyamapori kuingia kwenye maeneo ya watu, huchangia migongano na kuisihi.

Katika hilo anaeleza kwamba hata wadau wanapoandaa mikakati ya kuikabili hali hiyo, daiam wanapaswa kushirikisha wanavijiji jirani wafahamu n aina za taarifa zinazokosekana, pia zinazohitajika kutiliwa mkazo katika eneo husika.



# 'Vijana mjikinge na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi'

**Na Mwandishi Wetu,**
SINGIDA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga amewataka wazazi kuwaelimisha vijana namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), kutokana na kuwapo na kasi ya maambukizo kwa kundi hilo.

Nderiananga alitoa ushauri huo jana kwenye ziara ya Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI mkoani Singida, walipotembelea konga ya watu wanaoishi na maambukizi ya VVU (WAVIU) ya Halmashauri ya Singida Vijijini, ikiwa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na wadau kupitia Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS).

Alisema kuwa licha ya maambukizi ya VVU kupungua lakini kwa kundi la vijana na hasa kwa wasichana bado kasi ya maambukizi inaongozeka, hivyo wazazi na walezi hawana budi kutoa elimu kwa vijana ili kupata hamasa ya kupima afya zao.

"Tuwaelimishe vijana namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU, pia wasisitizieni wakapime wafahamu afya zao iwapo watakutwa na maambukizi watashauriwa kuanza dawa mapema," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inatoa dawa bila malipo na dawa zipo za kutosha kwa ajili ya wananchi wake ili wawe na afya bora.

Aidha aliwahimiza wanaume kufanya maamuzi ya kwenda kupima afya kwa kuwa taarifa za awali za Utafiti wa Viashiria vya Ukimwi ya Mwaka 2022/23 zinaonesha mwamko wa wanaume kupima afya bado upo chini.

"Nawaasa kinababa nendeni mkapime afya zenu, ukikutwa na maambukizi utaanza kutumia dawa na utaishi kwa malengo," alihimiza.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Nyongo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kwa ajili ya huduma za afya ambazo zinawezesha Watanzania kuwa na afya bora.

Pia alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Singida kwa kukusanya mapato ya ndani na kutenga fedha asilimia 10 kwa ajili ya kutoa mkopo wenye riba nafuu kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Suala la UKIMWI ni mtambuka na ndiyo maana likawekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali, hivyo wizara zote ni lazima kutekeleza shughuli za UKIMWI," alisema Nyongo.

Mwenyekiti wa Konga ya Halmashauri ya Singida Vijijini, Selemani Linja, alisema konga hiyo inatekeleza afua za UKIMWI kwa kushirikiana kwa karibu na uongozi wa halmashauri na wadau mbalimbali kwa lengo la kuratibu masuala yanayohusu watu wanaoishi na VVU.

"Shughuli tunazozifanya ni kuhamasisha jamii kupima afya kwa hiari, kutoa elimu ya VVU na ufuasi sahihi wa dawa kwa WAVIU, kupinga unyanyapaa kwa WAVIU, kuwakilisha WAVIU vijana na watu wazima katika majukwaa mbalimbali ya mwitikio wa UKIMWI ikiwa ni pamoja na kamati za kudhibiti UKIMWI ngazi zote pamoja na kuunda vikundi vya WAVIU kwa lengo la kutoa elimu rika ya matumizi ya huduma za tiba na matunzo na kuinuana kiuchumi," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela aliahidi kuzingatia ushauri na maelekezo ya kamati hiyo kwenye utekelezaji wa shughuli za mwitikio wa UKIMWI nchini.



Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni binafsi za Ulinzi Tanzania (UKUTA), Amani Mbijima (katikati), akiongoza mkutano wa kitaifa wa umoja huo, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja huo, Julieth Lushuri na Katibu wa Umoja huo, Abel Ndedwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Serikali yatoa bil.70/- utekelezaji miradi Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh.bilioni 70 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jimbo la Singida katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2023/24.

Mbunge wa Jimbo la Singida, Mussa Sima aliyasema hayo jana katika mkutano wa hadhara wa wananchi wa Kata ya Kisaki Wilaya ya Singida Mjini alipokuwa akisikiliza kero zao.

Sima alisema fedha hizo zimetekeleza miradi ya maendeleo katika kata zote za Jimbo la Singida na kusaidia kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Alisema fedha hizo zimepelekwa kwenye miradi ya barabara, afya, elimu na miradi ya maji.

Aidha, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jimbo la Singida Mjini.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria mkutano huo wa hadhara waliiomba serikali kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili hasa miundombinu ya barabara.

Walisema baadhi ya barabara hazipitiki kutokana na kuwa mbovu sana hasa kipindi cha masika.

Aidha, alisema kuna baadhi ya maeneo bado yanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama hali inayosababisha kufuata maji umbali mrefu.

Suala la umeme pia waliomba serikali kuhakikisha vitongoji vyote vya Kata ya Kisaki vinapatiwa umeme ambao utawasaidia kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

# Sukari yashuka bei mfungo Ramadhani, yauzwa 2,900/-

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI waumini wa dini ya Kislamu wakiwa wameanza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, bei ya sukari mkoani Singida imeshuka kutoka Sh.4,500 hadi Sh.2,900 kwa kilo kwenye maduka ya rejareja.

Kushuka kwa bei hiyo kumeleta unafuu kwa wananchi wa mkoa huo ambao baadhi yao walikuwa wakilazimika kutumia chumvi kama kiungo kwenye uji, kutokana na kushindwa kumudu bei hiyo na kuadimika.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika Manispaa ya Singida umebaini kwenye maduka ya rejareja kilo moja ya sukari inauzwa kwa Sh.2,900, na bei ya juu ni Sh.3,200.

Mmoja wa wafanyabiashara katika eneo la Ginnery, Athuman Idd alisema wamepunguza bei na kuuza kulingana na bei elekezi iliyotolewa na serikali baada ya maduka ya jumla nayo kuwapunguzia bei. Mfanyabiashara mwingine wa duka la rejareja eneo la Mandewa, Amina Haji,alisema hivi sasa kwenye maduka ya jumla wanauziwa Sh.140,000 kwa mfuko wenye ujazo wa kilo 50 sawa na bei ya Sh.2,800 kwa kilo moja.

"Kwa bei tunayouziwa na wafanyabishara wa maduka ya jumla hata niliuza kilo kwa Sh.3 000 napata faida ya Sh.10,000 kwa mfuko wa kilo 50 kwa hiyo inatosha," alisema.

Katika hatua nyingine, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wilaya ya Dodoma limewataka wafanyabiashara kutotumia fursa ya mwezi mtukufu wa Ramadhani kupandisha bei za bidhaa mbalimbali zinazotumika kwenye mfungo ikiwamo sukari. Mwenyekiti wa baraza hilo, Bashuru Omary, alisema kuwa wakipandisha bei za bidhaa hizo watakuwa wanawaumiza waumini ambao wanaofunga, lakini kipato chao ni kidogo kulinganisha na wengine wenye uwezo.b

Mmoja wa wafanyabiashara, Paskal Mariki, alisema kuwa watahakikisha bidhaa wanazouza kwa ajili ya matumizi ya mwezi mtukufu waumini wenye kipato cha chini wanamudu kununua.

**Imeandaliwa na Thobias Mwanakatwe na Peter Mkwavila**





## Wanafunzi 130 sekondari kuwezeshwa elimu bure

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI zaidi ya 130 wanaotoka katika mazingira magumu mkoani Mbeya watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha tano na sita mwaka huu wanatarajiwa kunufaika na fursa mbalimbali ikiwemo kununuliwa sare na vifaa vya shule pamoja na kusomeshwa.

Msaada huo unatarajiwa kutolewa na Mkurugenzi wa Shule za Paradise Mission ya mkoani Mbeya na Patrick Mission ya jijini Dar es salaam, Ndele Mwaselela ikiwa ni sehemu ya kuiunga mkono serikali kuboresha sekta ya elimu nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mwaselela ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa, alisema anakusudia kutoa misaada hiyo mwaka huu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kati ya wanafunzi hao, 100 watanunuliwa sare za shule na vifaa vya shule pamoja na kuwalipia bima ya afya ambayo itawasaidia miaka miwili.

Mwaselela alisema wanafunzi wengine 30 watasoma bure katika shule yake ya Patrick Mission ya jijini Dar es salaam kuanzia kidato cha tano mpaka cha sita.

"Mwaka huu ambao Rais Samia anatimiza miaka mitatu madarakani ni mwaka ambao hata shule yetu ya Paradise Mission itakuwa inatimiza miaka mitatu tangu ilipoanza, kwa hiyo tunataka kumuunga mkono Rais Samia kutokana na namna alivyoboresha mazingira ya elimu nchini," alisema Mwaselela.

Alisema kwa sasa serikali inatekeleza sera ya elimu bila malipo kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha sita hali ambayo imesaidia kupunguza matabaka kati ya watoto wa matajiri na masikini.

Alisema mpaka sasa zimeandaliwa timu maalumu za kwenda kuwatafuta watoto hao kwenye kata mbalimbali za Mkoa wa Mbeya ambao watanufaika na misaada hiyo.

Hivyo, aliwataka viongozi wa vijiji na kata kusaidia kutoa taarifa za watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili kuhakikisha wanapatikana watoto sahihi badala ya kuchomekwa watoto wanaotoka kwenye familia zenye uwezo.

Mwaselela ambaye kwa muda mrefu amekuwa mdau wa maendeleo mkoani Mbeya amekuwa akisomesha watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu wakiwemo yatima ambapo mpaka sasa anadai amesomesha zaidi ya watoto 500 ambao baadhi yao wamefika elimu ya juu.

# Wakulima wa chai walia kucheleweshewa malipo

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

WAKULIMA wa chai wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wamelalamikia wanunuzi wa zao hilo kuchelewesha malipo yao kwa zaidi ya miezi miwili, hali ambayo inawasababishia ugumu wa maisha na kushindwa kuhudumia zao hilo.

Wakulima hao wanawalalamikia wamiliki wa kiwanda cha chai cha Katumba kilichoko wilayani hapa wakidai kuwa ndicho kinakusanya majani yao na kuchelewa kuwalipa fedha zao hali ambayo inawasababishia usumbufu.

Mmoja wa wakulima hao, Feby Kijombe ambaye ni mkazi wa Bonde la Mwakaleli alisema wanunuzi hao walichukua majani yao tangu Disemba mwaka jana, mpaka sasa bado hawajalipwa na kila wakifuatilia wanapigwa kalenda.

Alisema wamewekeza nguvu kubwa kwenye kilimo cha chai, kwamba wanategemea wakilipwa fedha zao ndio wazitumie kununua chakula, lakini wanapocheleweshewa malipo wanasababishiwa matatizo mengine ikiwemo njaa.

"Mara ya mwisho tumefanya nao mkutano pale Mbeya na wakatuahidi kwamba watatulipa Machi 20 mwaka huu lakini kutokana na tulivyosumbuana nao hatuna imani kwamba watatulipa fedha hizo, sasa hivi tunashindwa hata kununua chakula watoto wanashindia mahindi ya kuchoma," alisema Feby.Therezia Mahenge alisema kutokana na usumbufu ambao wanaupata baadhi wameamua kutelekeza mashamba ya chai bila kuhudumia na wamekimbilia kwenye mazao mengine hali ambayo inatishia uwepo wa zao hilo.

Alisema kwa sasa vibarua wa kwenda kuchuma chai hawapo kutokana na wakulima kutokuwa na fedha za kuwalipa akidai kuwa vibarua wanataka malipo mapema wakati wao bado hawajalipwa fedha zao na mnunuzi. Alisema kuna baadhi ya watu ambao wanajiita kuwa ni viongozi wa wakulima lakini wao hawawatambui na kwamba wanafanya kazi kama madalali wa zao hilo.

"Sisi tunaamini kwamba kiongozi ni mtu anayekusaidia lakini sasa hawa wanaojiita viongozi, huku kwetu hawana msaada wowote, hawa ni wauaji kwa sababu hawatusaidii chochote zaidi ya kutunyonya wakishirikiana na mwekezaji," alisema Therezia.

Jeremiah Ngusa alisema awali wakati wanaanza kulima zao hilo walikuwa waliunda umoja uliokuwa unaitwa Umoja wa Wakulima Wadogo wa Chai ambao ulikuwa unasababisha tija kwao tofauti na mfumo wa sasa ambao wanashindwa kuuelewa.

Alisema kwa sasa wanatumia mfumo wa vyama vya ushirika ambao umeonekana kuzalisha matatizo mbalimbali kwenye kilimo cha zao hilo.

Mwenyekiti wa kamati ndogo ya ufuatiliaji wa madeni hayo, Ambilikile Mwasameta alisema wakulima wanaodai fedha zao kwenye kiwanda hicho wapo zaidi ya 13,000, wanadai viwango tofauti vya fedha kutokana na wingi wa majani waliyovuna.

Alisema wamekuwa wakihangaika kufuatilia bila mafanikio na kwamba kwa sasa wameshamwandikia barua Mkuu wa Wilaya hiyo, wabunge wa majimbo yote mawili ya wilaya hiyo na kwa mmiliki wa kiwanda lakini zote hazijajibiwa.

Mtendaji Mkuu wa viwanda vya Katumba na Tukuyu ambavyo vinalalamikiwa, Leby Gabriel alikiri kudaiwa na wakulima hao na kwamba wamekuwa wakiwalipa kwa awamu ambapo mpaka sasa wameshawalipa Sh. milioni 779 ambazo zililipwa Desemba. Alisema sababu zinazowafanya wachelewe kuwalipa wakulima ni kuyumba kwa soko la zao hilo hali ambayo imesababisha mapato kushuka.

Alisema wanaendelea na taratibu za kuhakikisha wanalipa fedha zote wanazodaiwa ili kuondoa migogoro ambayo haina tija kwenye kilimo cha zao hilo.



Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Tulia Trust, Joshua Mwakanolo (kulia), akipeana mkono na mmoja wa wanawake wenye ulemavu mkazi wa Kata ya Uyole, jijini Mbeya jana, walionufaika na msaada wa viti mwendo vinavyotolewa na taasisi hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Njombe yaongoza vifo vya watoto vitokanavyo na uzazi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete amesema Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa vifo vya watoto wadogo vitokanavyo na uzazi usio salama.

Aliyasema hayo wakati akisoma taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria iliyofika kukagua jengo la kinamama na watoto lililojengwa na wananchi na kukamilishwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Kikwete alisema katika Mkoa wa Njombe moja ya shida kubwa ambayo wananchi wanayo ni afya ya uzazi hasa kwa watoto wadogo. Alisema kumekuwa na vifo vya mara kwa mara vya watoto ambavyo wakati mwingine vimesababisha hata idadi ya wananchi mkoani Njombe kuwa ndogo sana.

"Kumbukumbu na takwimu zinatuonyesha kwamba katika moja ya mkoa ambao unaongoza kwa vifo vya watoto ni mkoa huu wa Njombe," alisema Kikwete.

Aidha alisema habari hiyo inasikitisha na ndiyo sababu Rais Samia Suluhu Hassan aliamua kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi ili kusaidia wananchi wa mkoa huo kwa kunusuru vifo vya kina mama na watoto.

Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria, Joseph Mhagama alisema kwa miaka mitatu mfululizo Mkoa wa Njombe umeendelea kupiga hatua za kimaendeleo hasa katika uboreshaji wa huduma za afya kwenye Hospitali ya Mji wa Njombe.

Alisema Rais Samia yupo karibu na wananchi wa Njombe na Watanzania kwa kuhakikisha kuwa huduma za afya zinasogezwa karibu na wananchi na zinakuwa bora.

Diwani wa Kata ya Ramadhani, Nickson Nganyange aliiomba serikali kuwajengea wodi ya wazazi katika zahanati iliyopo mtaa wa Ramadhani na Wikichi katika Halmashauri ya Mji wa Njombe kwakuwa huko nako kuna changamoto ya vifo vya watoto.



# SMZ yaondoa marufuku uingizaji ndizi kutoka Bara

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeruhusu uingizwaji wa ndizi sambamba na kuchukua tahadhari juu ya magonjwa yanayoathiri zao hilo.

Zanzibar ilipiga marufuku uingizwaji wa zao hilo zaidi ya miaka kutoka Tanzania Bara.

Waziri wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo jana mjini Unguja wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya uingizwaji wa ndizi nchini kwa tahadhari maalum.

Alisema mwaka 2007 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza tahadhari ya kutoingiza mmea wa migomba ikiwemo ndizi, majani na kigogo kwa madhumuni ya kuvikinga Visiwa vya Zanzibar visishambuliwe na tatizo la maradhi ya mnyauko wa migomba.

Alisema ugonjwa huo ulikuwa umeshamiri katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Kagera, Bukoba na Mara.

Shamata alisema kuwa Serikali ilitoa taarifa ya maradhi hayo kwamba yana uwezo wa kuangamiza asilimia 100 ya uzalishaji wa zao hilo, hivyo iliomba kupatiwa ushirikiano kwa wadau ili kukwepa kuingiza maradhi hayo ndani ya Visiwa vya Zanzibar.

"Nataka niwaambie kuwa tahadhari hiyo iliyowekwa imesababisha kuwa na uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo sokoni kwa kipindi cha takriban miaka 17 jambo ambalo limesababisha changamoto kwa wakaguzi wa mazao, wafanyabiashara na wadau wengne katika utekelezwaji wa tahadhari hiyo" alisema Shamata

Alisema kuwa pamoja na tahadhari zinazoendelea serikali inaruhusu uingizwaji wa zao la ndizi kwa taratibu maalum ili kupunguza changamoto kwa mujibu wa Sheria ya Karantini ya Mmea na Mazao Namba 9 ya Mwaka 1997 kwamba serikali inaamuru kufuatwa utaratibu wa uingizwaji wa zao hilo.

"Tunaomba wafanyabiashara wanaoruhusiwa kufanya biashara ya ndizi wanatakiwa kusajiliwa na kupatiwa vibali maalum vya uingizwaji wa ndizi kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo sambamba na kuzipeleka bidhaa hizo kwa wakaguzi wa kitengo cha karantini na ukaguzi wa mazao kabla kuingiza nchini" alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis Juma aliwataka wote wanaohusika na uingizwaji wa zao hilo kufuata taratibu zilizowekwa na Serikali pamoja na wananchi kufahamu hali halisi iliyopo kwa lengo la kutoa ushirikiano katika kudhibiti uingizwaji wa maradhi nchini.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi wamepongeza hatua hiyo wakisema itasaidia kupungua kwa bei ya ndizi hasa katika kipindi hiki cha Ramadhani ambapo mahitaji ya ndizi ni makubwa.

# TMA Zanzibar yatoa tahadhari ujio mvua za masika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Kanda ya Zanzibar imewataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na mvua za masika zilizoanza kunyesha.

Tahadhari hiyo imetolewa jana visiwani hapa na Kaimu Mkurugenzi Mamlaka ya Hali ya Hewa Kanda ya Zanzibar, Masuod Makame Faki, wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya ujio wa mvua za masika mwaka huu.

Alisema mvua hizo ambazo zimeendelea kunyesha kwa wiki ya pili katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Zanzibar zinatarajiwa kuisha katika wiki ya tatu ya Mei 2024 kwa kiwango cha wastani na juu ya wastani.

Akizungumzia athari ambazo zinaweza kujitokeza alisema kuwa ni vipindi vifupi vya mvua kubwa zinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko, magonjwa na athari mbalimbali, hivyo aliitaka jamii kuchukuwa tahadhari mapema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Makame Khatib Makame alisema kamisheni hiyo inaendelea na mikakati yake ikiwemo kutoa elimu kwa wananchi ili kuchukua tahadhari mapema ya kujikinga na athari za mvua hizo.

Aidha, aliwataka wavuvi na watumiaji wa bahari kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzifanyia kazi ili kuepukana na maafa yanayoweza kujitokeza wakiwa katika shughuli zao.

Pia aliwataka wananchi wanaoishi sehemu hatarishi ikiwemo pembezoni mwa mito na kwenye njia za maji kuchukua tahadhari mapema kabla ya kufikwa na maafa katika maeneo yao.




Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah (katikati), akipokea tuzo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kutoka kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, jijini Zanzibar juzi, iliyotolewa na Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), kutokana na juhudi zake za kutambua mchango wa Wanawake katika maendeleo. Kulia ni Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Silla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwanja wa Ndege Abeid Karume waibuka kidedea Afrika

**Na Rahma Suleiman,**

UWANJA wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) Zanzibar, umeshinda tuzo ya uwanja bora wa ndege Afrika. AAKIA umeshinda tuzo hiyo ikiwa ni uwanja unaotoa huduma bora kwa abiria chini ya watu milioni mbili kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Seif Abdalla Juma tunzo hizo zinazotolewa na Baraza la Kimataifa la Viwanja vya Ndege ambapo zimetangazwa Machi 11 mwaka huu.

Mkurugenzi huyo alisema tuzo za kila mwaka za huduma bora za viwanja vya ndege zinatambua ubora wa uwanja wa ndege kupitia maoni ya abiria duniani.

Alisema maoni hayo yanayopatikana kwa utafiti maalumu unaofanywa kila siku kwa abiria katika maeneo wanayoondoka na kuwasili katika vipengele mbalimbali ikiwemo utendaji bora wa wahudumu, wepesi wa safari kwa abiria, huduma zenye kukidhi matakwa ya mteja na usafi wa majengo ya abiria.

"ZAA ilijiunga rasmi na kuwa mwanachama wa ACI Oktoba 2022 kwa madhumuni ya kujipima huduma zake kwa abiria katika kipengele cha abiria wanaondoka kwa watendaji wake kupatiwa mafunzo rasmi na baraza hilo ambapo ilianza kupata matokeo bora zaidi ya ujumla kuanzia robo ya kwanza ya mwaka 2023 kwa kuwa namba tano kwa utoaji wa huduma kati ya viwanja 17 vya ndege Afrika" alisema.

Aidha alisema mamlaka inatarajia kukabidhiwa rasmi tuzo hiyo Septemba 25 mwaka huu katika mkutano na maonyesho ya kila mwaka ya huduma kwa wateja duniani yatakayofanyika Atlanta nchini Marekani.

"Natumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kufungua milango ya mashirika na kampuni kubwa za kimataifa yenye uwezo na uzoefu wa uendeshaji na utoaji wahuduma katika viwanja vya ndege," alisema.

Hata hivyo alitoa pongezi na shukrani kwa wafanyakazi na wahudumu wote wa sekta ya umma na binafsi kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uzalendo.

Pia aliyapongeza mashirika ya ndege ya ndani na ya kimataifa, pamoja na wadau wote wa sekta ya anga na utalii.

Alisema: "Tumedhamiria kuendelea kujikita katika ulimwengu wa ushindani kwa kutathmini na kupima ubora wa huduma zetu kwa kila hatua ili kutimiza azma yetu ya kuwa kinara wa huduma bora za viwanja vya ndege barani Afrika ifikapo mwaka 2027".

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**PILI IBRAHIM LEGUNA** anatangaza kupotelewa na **CERTIFICATE IN COMMUNITY HEALTH** chenye namba **NS/4822/0021/2014** kilichotolewa na NEEMA HUHAI NEW MAFINGA mwaka 2017 pamoja na Transcript ya matokeo. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/KIL/1873/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BOAZ JAMES LIHAWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1578/0068** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia CHANGARAWE SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/24974/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HAMAD ENZLON MAGOLI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA **"PASSPORT"** YENYE NAMBA TAE 322062. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA NYARAKA IYO YA HATI ATOE TAARIFA KUTUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/2774/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LUGENGA MOHAMED MAYILAGUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 176 DFS** aina ya **KINGLION.** Chassis namba **L7GPCKYLY3M1389321.** Engine namba **KL1571MJ 2 M51389321.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: ***NJ/TR/RB/227/2023.***

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAIS NDIGUTI MOLLEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 786 BZK** aina ya **TOYOTA IST** yenye Chassis namba **2NZ2793575.** Engine namba **NCP600107700.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/3721/2024.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT ARUSHA**

**MISC. COMMERCIAL APPLICATION NO. 1 OF 2024**
**(Original from Commercial Case No 3 of 2022)**

**STEPHEN MAHENDEKA MGANGA ...............................APPLICANT**

**VERSUS**

**BEST WAY CAPITAL MANAGEMENT LIMITED..........RESPONDENT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO:**
**Managing Director,**
**Best Way Capital Management Limited,**
**P.O.Box 105395,**
**DAR-ES-SALAAM,**

**TAKE NOTICE** that the Applicant has instituted a suit against you with particulars of claim set out in the application filed in this Court. Service of the Summons on you has been ordered by means of this publication, You are directed to collect copies of the summons and application from the Court's Registry, P.O.Box 3140 Arusha.

You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 1st day of April, 2024 at 10:00 a.m.when this application will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, should you default to enter appearance in Court on the day and time mentioned above, the case will proceed and ruling may be given in your absence.

Given under my Hand and the Seal of the Court this 06th day of March, 2024

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa Dar es salaam**

**Shauri la Mirathi Na. 363/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ADAM ABDALLAH LUPATU WA KINONDONI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA SHEILA ADAM LUPATU**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 mwezi 04 mwaka 2024 kabla hiyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Limetolewa leo tarehe 13 Mwezi 03 Mwaka 2024.

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 4779 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: KAROLI ELIAS CHANZE**

**By 1: GETRUDE KAROLI CHANZE**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 26 day of March.2024

Dated at Morogoro this 08 day of March.2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and administration Cause No 5220 of 2024**

**In the matter of the estate of the late SAIMON NGOSI MATOTANJE of Chamwino within Dodoma Region**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by POLIAS SAIMON NGOSI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of 4...................... 2024

Dated at Dodoma this 13 day of 3...............2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KIBAIGWA AUCTION MART**
**P.O.BOX 20,**
**DODOMA**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KIBAIGWA AUCTION MART,

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA GARI MOJA AINA YA Toyota Land Cruiser PRADO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 668 EDL MALI YA ALOYCE JOHN KAMAMBA , BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 22/03/2024 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**

---

**MWAMBA MILLENNIUM COMPANY LIMITED**
**P.O. Box 3221 - DODOMA**

## TANGAZO TANGAZO MNADA WA HADHARA Shauri la Ndoa No. 18/2022

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Kondoa Mjini, Tutaendesha Mnada wa hadhara wa kuuza Nyumba iliyopo Mtaa wa Mnarani kiwanja No. 90 kitalu 'AA', Mali ya wanandoa, **ADAM RAMADHANI AWADHI NA HADIJA RAMADHANI HAYMA** mgawanyo wa talaka. Mnada utafanyika tarehe 25.03.2024 siku ya Jumatatu saa tano kamili asubuhi (05:00). Huu mnada utafanyika Soweto Mtaa wa Mnarani.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnunuzi atalipa 25% na atamalizia ndani ya siku 14 Malipo75% ya bei itakayowekwa kwenye mnada.
3. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake
4. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu namba **0712 245 977, 0784 155 866, 1767 245 977.**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

Pastory H. Kaboya
Mkurugenzi

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARIKIMATAIFA

# Juhudi kupeleka chakula Gaza zazidi kuongezeka

**GAZA, Palestina**

BOTI zilizobeba shehena ya misaada ya chakula zinaelekea eneo la Ukanda wa Gaza, kwa ajili ya kuwasambazia Wapalestina wanaohangaika kutokana na janga la njaa.

Zoezi hilo lilianza jana baada ya boti ya kwanza kutia nanga katika pwani ya mji wa Gaza ikiwa na shehena ya chakula tani 200. Nchi mbalimbali ikiwamo Marekani zinaongeza juhudi ya kupeleka msaada zaidi ya kibinadamu katika eneo hilo lililozingirwa na Israel.

Hata hivyo, shirika la msaada la Umoja wa Mataifa lililoko Gaza, lilisema Israel ilishambulia maghala yake ya chakula katika mji wa Kusini wa Rafah na mfanyakazi wake mmoja aliuawa.

Baadae jioni Israel ilitoa taarifa ikisema ilimuuwa kamanda wa kundi la Hamas,Mohammed Abu Hasna kwenye shambulio la roketi dhidi ya kituo cha kusambaza chakula cha Umoja wa Mataifa.

Maofisa wa afya wa Palestina waliripoti kwamba watu wengine wanne akiwamo mfanyakazi wa umoja wa Mataifa waliuawa.

Mataifa wafadhili na mashirika ya hisani yalieleza kwamba yanaendelea kupeleka msaada wa chakula katika Ukanda wa Gaza ambao una zaidi ya watu milioni 2.4 wanaohitaji msaada wa dharula.

Mpaka sasa njia pekee ya kufikisha msaada wa chakula ni kutumia njia ya kudondosha kwa ndege ambayo ni misaada michache inayowafikia walengwa.

Juhudi za kufunguliwa njia ya baharini zimeonesha haina uhakika kutokana na msaada huo wa kiutu kulazimika kupitia njia ya barabara ambayo si salama.

Mtazamo huo, uliotolewa na mashirika 25, ikiwamo la haki za kibinadamu la Amnesty International na Oxfam, ulisema katika mji wa Gaza Wapalestina wanaonekana kukata tamaa huku wakiwa na matumaini ya kuwasili kwa boti ya msaada ya shirika la hisani la Open Arms.

Juzi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Cyprus, Constantinos Kombos, alisema meli nyingine ya pili ya msaada ambayo ni kubwa zaidi ilikuwa ikijiandaa kuelekea Gaza.

Kombos pia alifanya mazungumzo kwa njia ya mtandao na Waziri wa mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, na mawaziri na maafisa wa ngazi za juu kutoka Uingereza,Umoja wa Falme za kiarabu,Qatar,Umoja wa Ulaya na Umoja wa Mataifa katika kujadili suala la kutumia njia ya baharini.

Alisema viongozi wote walikubaliana njia bora zaidi kwa sasa ni ya barabara kupitia Misri na Jordan ambayo inaingia Israel hadi Gaza.

Mpaka sasa juhudi hizo za upatinishi zimeshindwa kupata makubaliano mapya ya kusitisha vita na waziri wa ulinzi wa Israel Yoav Gallant ameapa kwa mara nyingine kwamba vikosi vya nchi hiyo vitaingia kila kona ya Gaza kutimiza azma yao ya kuliangamiza kundi la Hamas.

Wakati huohuo Marekani inatarajiwa kutangaza vikwazo vipya kuhusiana na vituo viwili vilivyojengwa kinyume cha sheria na walowezi wa kiyahudi katika maeneo mawili ya Ukingo wa Magharibi.

Vituo hivyo vinatumika kama ngome za mashambulizi ya walowezi wa Israel wanaotajwa kuwa na itikadi kali. Vikwazo hivyo vinatarajiwa kutangazwa jana.

***BBC***




Mwanamama akimsaidia mwanamume aliyejeruhiwa, nje ya hospitali ya al-Najjar eneo la Rafah, kusini mwa Ukanda wa Gaza, kufuatia shambulio la Israeli. **PICHA: AFP**

# Ndege za KLM kubana matumizi kwa abiria

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKA la Ndege la KLM limetambulisha mfumo mpya wa kubana matumizi ya chakula unaofahamika kama AI kwa wasafiri wake.

Mfumo huo mpya utakuwa na uwezo wa kukadiria kwa usahihi kiasi cha chakula kwa kila safari ya ndege, una lengo la kupunguza upotevu wa chakula kutokana na asilimia tatu mpaka tano ya abiria hawafiki katika safari zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo, mfumo huo unaongeza ufanisi kwenye suala la huduma bora kwa abiria.

Akizungumzia mfumo Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi mwenza wa kampuni hiyo, Sander Stomph, alisema muungano huo wa huduma hiyo utatoa tija kwa maboresho ya huduma za KLM.

"Tunafuraha kwamba tumeweza kutoa mchango muhimu katika mradi huu muhimu wa KLM. Lengo letu na Kickstart AI ni kuharakisha kupitishwa kwa AI katika jumuiya ya wafanyabiashara na tunatazamia kufanya kazi kwa karibu na makampuni mengine," alisema.

Aliongeza: "Mfumo mpya unaanza kufanya kazi kuanzia siku 17 mpaka dakika 20 kabla ya kuanza kwa safari husika, hii inamaanisha kuwa idadi sahihi zaidi ya abiria inatabiriwa kwa mchakato mzima na kupunguza au kuodoa kabisa ziada ya chakula,"

Sander alisema utafiti wao wa miezi mitatu wa mfumo huo umeonyesha hapo awali chakula kwenye kila safari kinapoteaa kwa asilimia 63 ukilinganisha na mfumo mpya wa kila abiria kuandaliwa chakula chake.

**"Tunafuraha kwamba tumeweza kutoa mchango muhimu katika mradi huu muhimu wa KLM. Lengo letu na Kickstart AI ni kuharakisha kupitishwa kwa AI katika jumuiya ya wafanyabiashara na tunatazamia...**

# Uganda kutumia Dola mil 800 kueneza Kiswahili

**KAMPALA, Uganda**

SERIKALI ya Uganda, imetenga dola za kimarekani milioni 800 (Euro milioni 625), kwa ajili ya kukuza na kufundisha lugha ya Kiswahili nchini humo.

Imesema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za kuimarisha ushirikiano wa kikanda.

Watumishi wa umma wakiwamo madaktari, wauguzi na wafanyakazi wa mpakani, watapewa kipaumbele katika programu ya mafunzo ya Kiswahili.

Programu hiyo bado haijazinduliwa. Waziri wa Uganda wa Masuala ya Afrika Mashariki, Rebecca Kadaga, alisema.

Waziri huyo, hakutoa maelezo zaidi, kuhusu lini na jinsi gani programu ya mafunzo itazinduliwa.

Kama sehemu ya juhudi za kueneza lugha hiyo nchini, Kadaga alisema maofisa wote wakuu serikalini, wakiwamo mawaziri na majaji, watasoma masomo ya lazima kila wiki.

Julai 2022, serikali ya Uganda iliidhinisha kupitishwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi na kuagiza kuwa somo la lazima katika shule za msingi na upili.

Lakini lugha hiyo, kwa sasa inafundishwa katika shule chache za sekondari nchini.

Takriban watu milioni 200 wanazungumza Kiswahili duniani na mwaka wa 2021, lugha hiyo ilipata msukumo mkubwa zaidi pale Umoja wa Mataifa (UN), ulipoteua Julai 7, kila mwaka, kuwa Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani.

Pia ni lugha hiyo, ni rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Mwaka 2019, Kiswahili kilikua lugha pekee ya Kiafrika kutambuliwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Pia kuna juhudi za kuitambulisha katika

HABARI MICHEZO

# AMPUTEE ZANZIBAR YAJITOA RASMI MICHUANO YA AFRIKA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa ya Amputee ya Zanzibar (Karafuu Empire), haitashiriki katika mashindano ya Afrika ya mchezo huo mwaka huu kwa sababu ya kukosa uanachama kamili wa Shirikisho la Amputeee Afrika (CAAF), imeelezwa.

Nchi 16 wanachama wa CAAF zinatarajiwa kuchuana katika mashindano hayo ya mwaka huu yatakayofanyika mwezi ujao katika jiji la Cairo, Misri.

Mwaka 2021, Zanzibar ilishiriki mashindano hayo kwa mara ya kwanza yaliyofanyika Dar es Salaam, kama timu iliyojitegemea.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu Zanzibar (ZAFF), Hassan Silima, alisema hawatashiriki mashindano hayo kwa sababu bado hawajakidhi vigezo vya kupata uanachama kamili CAAF na Shirikisho la Dunia la mchezo huo.

Silima alisema awali ZAAF ilipata uanachama wa muda wa miaka miwili na kupata fursa ya kushiriki mashindano ya mwaka 2021 huku wakitakiwa kukamilisha mchakato wa kuwa mwanachama kamili.

Alisema uwezekano wa ZAAF kupata uanachama kamili bado ni mgumu licha ya viongozi kuendelea na mchakato wa kuhakikisha wanatimiza vigezo ili wapate nafasi ya kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Aliongeza ugumu mkubwa unaowafanya wakose uanachama kamili ni Zanzibar kutokuwa nchi kamili inayotambulika na Umoja wa Mataifa kama ambavyo Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kukosa uanachama kamili katika mashirikisho ya kimataifa ya CAF na FIFA.

"Hatujavunjika moyo kwa kukosa uanachama, lakini sijui kama itawezekana, kwa sababu ili tuwe wanachama ni mpaka hawa CAAF wabadilishe katiba yao na isifanane na CAF wala FIFA, wawe na katiba ambayo nchi za Afrika kama zinazofanana na zetu tuweze kutambulika, hivyo ili jambo sio la leo lakini bado tupo katika subira," alisema Silima.

Aliongeza licha ya baadhi ya wachezaji kukata tamaa baada ya kukosa fursa ya kushiriki mashindano ya kimataifa, uongozi bado wanaendelea na jitihada za kuhakikishia wachezaji wanacheza kwa malengo.

"Baadhi ya wachezaji wamehisi kama wamerudi nyuma au kuvunjika moyo kwa sababu malengo yalikuwa ni kwenda kuonyesha uwezo na vipaji vyao katika mashindano hayo, wameumia baada ya kubaini sasa wataishia kucheza michuano ya ndani pekee," Silima aliongeza.

Wakati huo huo, wachezaji wa tatu kutoka Zanzibar wamechaguliwa katika Timu ya Taifa ya Amputee ya Tanzania ili kujiandaa na mashindano ya Afrika.



Mchezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya COSAFA yatakayofanyika hivi karibuni nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# Tembo Warriors yaitisha Rwanda

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu (Tembo Worriors), limesema hawahofii kukutana na Rwanda katika mchezo wa awali wa mashindano ya Afrika (CANAF) utakaochezwa Aprili 20, mwaka huu jijini Cairo, Misri.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka kambini Karatu, Arusha, Meneja wa timu hiyo, Zaharani Mwenemti, alisema kikosi chake hakina wasiwasi kuelekea mchezo huo kwa sababu wanamfahamu vizuri mpinzani wao.

"Si mara ya kwanza kukutana na timu hiyo, tunajua sehemu za kuwabana ili wasipate nafasi ya kuzifumania nyavu yetu, " alisema Mwenemti.

Aliongeza michezo miwili ya kirafiki waliyocheza itawasaidia kufanya vyema katika mechi hiyo ambayo wanatarajia itakuwa na upinzani mkubwa.

Alisema morali ya wachezaji wake iko juu na kuongeza wanaendelea kufanyia kazi mapungufu yao kabla ya kuanza safari ya kuelekea Misri.

Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salvatory Edward, alisema malengo yake ni kutwaa ubingwa wa michuano hiyo na anaamini na maandalizi ya muda mrefu waliyofanya yatawafanya wafikie malengo.

Salvatory alisema kambi yake imeimarika baada ya wachezaji wake, Shadrack Hebron na Ramadhani Chomelo, wanaocheza soka la kulipwa Uturuki kujiunga na wenzao.

Katika mashindano hayo, Tanzania iko katika Kundi D pamoja na Sierra Leone, Angola na wenyeji Rwanda.

## Kriketi wanaume wawasili Ghana

**Na Saada Akida**

WAKATI Timu ya Taifa ya Wanawake ya KriketI haijafanya vizuri kwa kumaliza katika nafasi ya nne kwenye mashindano ya All Africa Games, kikosi cha wanaume cha mchezo huo kimewasili leo Ghana kikitokea Malaysia tayari kupeperusha bendera ya Tanzania.

Timu ya Wanawake ya Kriketi ya Nigeria imemaliza katika nafasi ya kwanza, Afrika Kusini wakafuatia. Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Chama cha Kriketi Tanzania (TCA), Hamis Hassan, alisema sababu iliyowafanya wanawake washindwe kufanya vizuri ni kutokana na kikosi chao kuundwa na wachezaji wengi vijana.

"Bahati mbaya timu ya wanawake hatukuingia hatua ya nusu fainali, kiujumla timu ilikuwa vizuri, ilikuwa mpya katika mashindano ya All Afrika Games yaliyoshirikisha timu kubwa ikiwamo Afrika Kusini," Hassan alisema.

Aliongeza ana imani na kikosi cha wanaume kitafanya vizuri baada ya kutoka kushiriki mashindano ya 2024 Malaysia Open T20 Championship, na Tanzania imeingia katika orodha ya timu 12 zitakazowania tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Dunia.

## TWBA yajipanga kukutana Jumanne

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya Utendaji ya Chama cha Kikapu kwa watu wenye ulemavu (TWBA), inatarajiwa kukutana wiki ijayo kwa ajili ya kupitisha kalenda ya shughuli za chama hicho kama mwongozo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), linavyoelekeza.

Mwenyekiti wa TWBA, John Bandie, alisema kikao hicho pia kitajadili maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Chama cha Kimataifa cha Kikapu (TWBF) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro.

"Jumanne ya wiki ijayo tutakutana ili kupitia kalenda yetu, kwa ajili ya kuona kama inaendana na maelekezo tuliyopewa, tunaamini kikao hicho kitatoa dira ya kule tutakapoelekea," Bandie alisema.

Alisema moja ya mikakati yao ni kuhakikisha kila mkoa unakuwa na chama cha mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu na wanaiomba serikali iwasaidie kurahisisha usajili wa katiba zao.

Aliongeza TWBA inatarajia kuandaa bonanza litakalofanyika Aprili 12, mwaka huu kwenye viwanja vya Kidongo Chekundu, Dar es Salaam ambalo litawashirikisha wachezaji kutoka Shule ya Sekondari Jangwani.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inatayarisha dau la pauni milioni 80 ili kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford, na watakuwa tayari kumlipa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki. ***(Star)***

### DIAZ AKARIBIA PSG

PSG pia wanavutiwa na winga wa Liverpool, Luis Diaz, mwenye umri wa miaka 27 kama mbadala wa mshambuliaji wa Timu ya taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe (25), ambaye anatarajiwa kujiunga na Real Madrid. ***(El Pais)***

### LUKAKU, KEPA KUUZWA

MWENYEKITI wa Chelsea, Todd Boehly, yuko tayari kumuuza mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, ambaye yuko Roma kwa mkopo, na kipa wa Hispania, Kepa Arrizabalaga (29), aaliyeko pia kwa mkopo Real Madrid, kwa klabu za Saudi Pro League majira ya joto katika jaribio la kuongeza pauni milioni 100 kutokana na mauzo ya wachezaji. ***(Talksport)***

### BRANTHWAITE KUTUA UNITED

MANCHESTER United imeupa kipaumbele usajili wa beki wa kati msimu huu wa joto, huku mlinzi wa Juventus na Brazil, Gleison Bremer, mwenye umri wa miaka 26, akiwa juu kwenye orodha ya timu zinazomwania pamoja na mlinzi wa Everton (21), Jarrad Branthwaite. ***(i Sport)***

### GOMEZ KUITWA ENGLAND

MLINZI wa Liverpool, Joe Gomez, mwenye umri wa miaka 26, mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney (27) na kipa wa Rangers, Jack Butland (31), wanatajwa kujumuishwa katika kikosi cha England kitakachocheza dhidi ya Brazil na Ubelgiji wakati wa mapumziko ya kimataifa ya mwezi huu. ***(Sky Sports)***

### PSG KUMUUZA SIMONS

KLABU ya Paris St-Germain huenda ikamuuza kiungo wa Uholanzi, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko kwa mkopo RB Leipzig, kama sehemu ya mpango wa kubadilishana mchezaji wa Manchester City na Ureno Bernardo, Silva (29). ***(CaughtOffside)***

### BARCA KUMUUZA ARAUJO

BARCELONA inapania kumuuza mlinzi wa Uruguay, Ronald Araujo, mwenye umri wa miaka 25, ambaye amekuwa akihusishwa na Bayern Munich, ikiwa watapokea ofa ya euro milioni 100. ***(ESPN)***

### MILAN, MARTINEZ SAFI

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, hatarajii changamoto yoyote kati ya klabu hiyo ya Serie A na mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 26 kuhusu kuongeza mkataba wake. ***(Gazzetta dello Sport)***

### SCHULTE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inatazamia dili la kumnunua mlinda mlango wa Columbus Crew na Marekani, Patrick Schulte, mwenye umri wa miaka 23, iwapo kipa, Aaron Ramsdale (25), ataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto. ***(Telegraph)***

### CHELSEA YAMTAKA MUSIALA

CHELSEA ipo tayari kupata ada nzuri ikiwa Bayern Munich itakubali kumuuza kiungo wa kati wa Ujerumani, Jamal Musiala, ambaye anahusishwa na uhamisho wa pauni milioni 80 kutoka kwa wababe hao wa Bundesliga, huku Manchester City na Liverpool wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PSG YATENGA DAU JUU KWA RASHFORD

Nyota huyo anatajwa kwenda kurithi mikoba ya Mbappe...

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Marcus Rashford, anawaniwa katika usajili wa dirisha la majira ya joto ambapo Paris Saint-Germain inajipanga kutoa dau kubwa kumng'oa kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Rashford ametumia muda mwingi wa maisha yake akiwa na United, akijiunga na akademi ya vijana tangu akiwa na umri wa miaka saba na sasa amebakisha mechi saba tu kabla ya kufikisha michezo 400.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 yuko mbioni kuwapita magwiji kama David Beckham, Nobby. Stiles, Peter Schmeichel na Denis Law kwa kucheza mechi nyingi msimu huu.

Lakini uongozi mpya wa United unaweza kufanya uamuzi mkubwa juu ya Rashford ifikapo msimu wa joto.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2028 baada ya kusaini mpya mwaka jana, lakini gazeti la Daily Mirror limeripoti PSG wako tayari kutoa pauni milioni 75 katika kutafuta mbadala wa Kylian Mbappe.

Pamoja na Mbappe ataondoka pale Parc des Princes kama mchezaji huru kuelekea Real Madrid, PSG haitakosa fedha za kutumia kumnasa fowadi huyo anayeondoka atarudisha kiasi cha euro milioni 80 kwa klabu ambayo ni bonasi aliyokuwa amepewa.

Miamba hao wa Ufaransa hapo awali walikuwa wakimtaka Rashford mwaka juzi kabla ya kuwa na msimu bora zaidi wa maisha yake na kufunga mabao 30 katika mashindano yote.

Lakini msimu wa 2023/24 imekuwa hadithi tofauti kwa Rashford, amefunga mabao saba pekee katika michezo 27.

United inasemekana imetaja thamani ya Rashford ni pauni milioni 100.

Kumuuza Rashford kwa pauni milioni 75 kutamfanya kuwa mchezaji wa pili kuuzwa kwa bei kubwa kwa klabu hiyo, nyuma ya Cristiano Ronaldo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 80 wakati akitua Real Madrid mwaka 2009.

David Beckham, ambaye alijiunga na Madrid kwa pauni milioni 25 mwaka 2003, bado yuko nafasi ya tano.

# RAYA APIGIWA DEBE ARSENAL

**LONDON, England**

GWIJI wa soka wa Arsenal, Martin Keown, amependekeza golikipa, David Raya, kutoka nchini Hispania anatakiwa kuchukua mazima nafasi ya Aaron Ramsdale kama kipa chaguo la kwanza.

Arsenal wametinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kushinda kwa penalti dhidi ya FC Porto ya Ureno, huku kipa huyo akiibuka shujaa baada ya kuokoa penalti mbili.

Washikabunduki hao walimaliza ukame wa miaka 14 kufika hatua ya nane bora ya michuano hiyo mikubwa Ulaya.

Keown amesema baadhi ya mashabiki walikuwa hawaamini uwezo wa kipa huyo kutokana na mashaka naye hasa alipoanza kuaminiwa na Kocha, Mikel Arteta.

Raya, ambaye alijiunga na klabu hiyo kutoka Brentford kwa mkopo msimu wa joto, amechukua nafasi ya Ramsdale kama kipa chaguo la kwanza msimu huu.

"Kulikuwa na wasiwasi uwanjani alipoingia kwa mara ya kwanza katika timu ya Arsenal. Unaona sasa, kuna imani kwake na kuna umoja sasa," alisema Keown akiiambia TNT Sports.



## Ederson hatarini kuikosa Arsenal

**LONDON, England**

GOLIKIPA wa Manchester City, Ederson huenda akaukosa mchezo ujao wa Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal utakaopigwa Machi 31, mwaka huu.

Kipa huyo anahofiwa kuukosa mchezo huo ambao huenda ukawa sehemu ya maamuzi ya ubingwa msimu huu kutokana na kusumbuliwa na jeraha la misuli, ambalo litamweka nje kwa muda wa wiki nane.

Kipa huyo raia wa Brazil aliumia alipomchezea vibaya, Darwin Nunez, wakati City ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield na kusababisha penalti ambayo ilipigwa na Alexis MacAllister na kuwasawazishia Wekundu hao.

Ederson pia anatazwamiwa kukosekana katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Newcastle United ambao utapigwa kabla ya mapumziko ya kupisha michezo ya kimataifa.

Kwa mujibu wa BBC Sport, Man City wameifahamisha Brazil, Ederson hatakuwa fiti kwa michezo hiyo ya kimataifa, ambapo Selecao wanatarajiwa kucheza dhidi ya England na Hispania katika muda wa siku tatu.

Baada ya kurejea kwa Ligi Kuu England, Manchester City itawakaribisha Aston Villa Aprili 3, mwaka huu kabla ya kusafiri kusini mwa London kumenyana na Crystal Palace siku tatu baadaye.



## Tajiri United kumng'oa Nevez

**MANCHESTER, England**

TAJIRI mpya wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, huenda akaruhusu zaidi ya pauni milioni 100 zitumike katika dirisha lijalo la majira ya kijoto kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Benfica na Ureno, Joao Nevez.



Nyota huyo anadaiwa kuwa na kipengele kinachomruhusu kuondoka ikiwa timu inayomhitaji itatoa kiasi hicho. Mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika 2028.

United inataka kumsajili nyota huyo kwa ajili ya kuboresha eneo la ushambuliaji ili kushindana kwa asilimia zote msimu ujao.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka tovuti ya Mirror, tayari Kocha wa United, Erik ten Hag, ameshawasilisha ripoti inayoeleza aina ya wachezaji anaowataka kwa msimu ujao.

Mmoja kati ya mastaa hao ni Nevez ambaye usajili wake ukikamika huenda ukavunja rekodi ya usajili wa Paul Pogba aliyesajiliwa kwa pauni milioni 89 mwaka 2016 akitokea Juventus.

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAIVAA MASHUJAA IKIRUHUSU BAO KILA MECHI

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI ikiivaa Mashujaa FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Simba imeruhusu mabao 18 kutinga katika nyavu zake, ikiwa ni wastani wa kufungwa goli moja kila mchezo.

Simba imecheza michezo 18 kabla ya mechi ya leo na tayari imeruhusu idadi hiyo na kuweka rekodi mbaya zaidi katika misimu ya Ligi Kuu Bara hivi karibuni.

Idadi hiyo ya mabao imevunja rekodi ya magoli 17 waliyofungwa kwa msimu mzima uliopita ambapo iliruhusu idadi hiyo katika michezo 30.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amekiri hilo na kusema wanaendelea kulifanyia kazi.

„ Ni kweli kuna matatizo, inaoneka kila mechi ni lazima turuhusu bao, hii pia si nzuri kwetu, tunaendelea kufanyia kazi mapungufu yote yaliyoonekana, kuruhusu mabao mepesi, kutokukaba, na kuonekana kuridhika mapema na mabao,“ alisema Matola.

Akizungumzia mechi ya leo dhidi ya Mashujaa, Matola alisema haitakuwa rahisi kutokana na wapinzani wao wamebadilika na si kama walivyokuwa katika mzunguko wa kwanza.

Matola alisema wamekuwa wakifuatilia mapungufu ya wapinzani wao, hivyo watayatumia kwa ajili ya kupata ushindi na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

„Kiuhalisia ligi ni ngumu na suala la ubingwa bado upo wazi kwa sababu kuna mechi nyingi na aliyekuwa juu yetu anaweza kupoteza hivyo hatujakata tamaa, kikubwa ni kushinda na hasa katika mechi yetu ya kesho (leo) dhidi ya Mashujaa," alisema Matola.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohammed Abdallah 'Bares', alisema wao wamejipanga vizuri na watacheza kwa kuwaheshimu Simba, kwa sababu ni timu bora na imetoka kufanya vizuri katika michezo iliyopita ikiwamo ya kimataifa.

"Tunawaheshimu Simba, imekuwa ikifanya vizuri, ina wachezaji wazuri lakini wana udhaifu wao, tutayatumia mapungufu yao ili kujaribu kupata ushindi katika mechi ya kesho (leo)," alisema Bares.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ipo kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 42 wakati Mashujaa yenye pointi 21 iko katika nafasi ya 11.



Magolikipa wa Mashujaa FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA : MTANDAO**

# Tanzanite, Ethiopia ni hesabu, heshima

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite) inatarajia kukutana na Ethiopia katika mechi yake ya tatu ya hatua ya makundi ya mashindano ya All Africa Games ikihitaji ushindi pekee ili kuweka matumaini ya kusonga mbele.

Katika mchezo huo, Tanzania inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0, lakini pia ikiiombea Ghana iifunge Uganda na kupata nafasi ya kucheza hatua inayofuata.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema kikosi chake kipo tayari kwa mpambano ‚mzito' wa kuwania nafasi ya kusonga mbele.

Shime alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu Ethiopia imejeruhiwa katika mechi mbili zilizopita hivyo anajiandaa kukutana na ushindani utakaosababishwa na wapinzani kuhitaji heshima.

"Tumefanya maandalizi ya mwisho na kuwaeleza wachezaji wangu umuhimu wa mchezo huo, vijana wameahidi kupambana ili kupata matokeo mazuri," alisema Shime.

Nahodha wa Tanzanite, Irine Kisisa, alisema timu yao iko tayari na wachezaji wote wanatambua umuhimu wa mechi hiyo ambayo wanahitaji ushindi ili kutinga hatua ya nusu fainali.

Kocha wa Ethiopia, Yosef Dadi, alisema anajua utakuwa mchezo mgumu kwa sababu Tanzania ina kikosi bora ambacho anaamini kitawapa upinzani maradufu.

Dadi alisema timu yake haijafanya vizuri katika mechi zilizopita lakini wataingia kuwavaa Tanzanite kwa ajili ya kupata matokeo chanya.

## Benchika: Al Ahly wanaihofia Simba

INATOKA UK. 24

kuwashangaza Al Ahly," Benchikha alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, amesema kujuana kwa wachezaji wa timu zote mbili kunatokana na kukutana mara kwa mara, hali hiyo ndiyo kunaifanya mechi hiyo kuwa na ahueni kwao.

„Itakuwa mechi ngumu sababu ya timu kujuana, lakini pia inatupa ahueni kwetu, wachezaji hawana presha nao, hivi karibuni tu tumecheza Cairo kwenye African Football League," alisema Kajula.

Miezi mitano iliyopita, Simba na Al Ahly walikutana katika mashindano mapya ya African Football League na Wekundu wa Msimbazi iliondolewa kikanuni.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 21, mwaka jana, timu hizo zilitoka sare mabao 2-2 na waliporudiana Oktoba 24, mwaka huu zikatoka tena sare ya bao 1-1, na Simba kutolewa kwa kanuni ya mabao ya ugenini.

Pia zilikuwa pamoja kwenye hatua za makundi msimu wa 2018/19 zikiwa Kundi D na zote zikasonga mbele hatua ya robo fainali, Al Ahly ikiongoza kundi, Simba ikifungwa mabao 5-0 ugenini na kushinda bao 1-0 nyumbani.

Mara nyingine tena ilikuwa hatua ya makundi msimu wa 2020/21, kila timu ikishinda bao 1-0 nyumbani, zote mbili zikisonga mbele, Simba ikiongoza kundi hilo.

## Gamondi afunguka ubingwa Bara bado

INATOKA UK. 24

heshimu kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Bado sina uhakika wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu licha ya timu yangu kuendelea kupata alama tatu katika kila mechi tunayocheza, naendelea kukiandaa kimbinu kikosi changu ili kizidi kunipatia matokeo kila mchezo ukiwamo dhidi ya Azam FC, Simba pamoja na michezo yote iliyopo mbeleyetu," Gamondi alisema.

Aliongeza bado ‚joto' la ligi linaendelea kupanda na hajiaminishi moja kwa moja ana uhakika wa kushinda taji hilo.

„Licha ya kupata ushindi na kufunga mabao mengi katika kila mechi, kila mchezo tunaendelea kukutana na timu zinazotupa ushindani katika mzunguko huu wa pili," aliongeza kocha huyo.

Gamondi alisema kulingana na ugumu wa ligi hiyo hataidharau timu yoyote na kutoangalia udogo wa wapinzani wao, zaidi ya kutafuta pointi tatu zitakazowapeleka kufikia malengo yao.

„Tunatakiwa kupambana, wachezaji wajitume zaidi, hatuwezi kuridhika kwa kuwa tunaongoza ligi kwa alama saba ambazo ni ndogo sana katika mchezo wa mpira wa miguu," alisema Gamondi.

Yanga inaongoza ligi ikiwa na pointi 49 na keshokutwa watakutana na Azam FC iliyoko katika nafasi ya pili ikiwa na alama 44 kibindoni, lakini imecheza michezo miwili zaidi. Wekundu wa Msimbazi ambao leo wataikaribisha Mashujaa wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 42, lakini wamecheza michezo 18.

# Michezo

Ijumaa Machi 15, 2024

Nipashe


**PSG yatenga dau juu kwa Rashford** UKURASA 21



# BENCHIKA: AL AHLY WANAIHOFIA SIMBA

## ●●●Kocha huyo atamba wanajipanga kuwashangaza baada ya...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kurejea nchini kuendelea na kibarua chake, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema Waarabu hao wa Misri, Al Ahly ndiyo wanaihofia Simba na wamekuwa na presha kutokana na kupangwa kukutana kwa mara nyingine katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imepangwa kucheza dhidi ya Al Ahly katika ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mechi ya kwanza ikichezwa kati ya Machi 29 na 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano yakifanyika Misri kati ya Aprili 5 hadi 6, mwaka huu.

Akizungumza jijini, Benchikha, alisema Al Ahly inafahamu inakutana na mpinzani mgumu kwao, hivyo anatarajia mechi zote mbili zitakuwa na ushindani.

Benchikha alisema Al Ahly hawajapenda kukutana na Simba kwa sababu timu hizo zinafahamiana kama zinacheza ligi moja kutokana na ratiba kuwakutanisha mara kwa mara kuanzia hatua tofauti.

„Al Ahly wanajua wanakuja kukutana na mpinzani mgumu kwa kiasi gani, na Simba itakwenda kupigania nafasi ya kutinga hatua ya nusu fainali na sio kuhofia hadhi yao. Tunatakiwa kujipanga kwenda kuthibitisha kwa nini tupo katika klabu 10 bora Afrika kwa kushindana na klabu namba moja na bila hofu. Kila kitu kinawezekana, hatuna presha nao kwa sababu tunaijua na tutapambana nao,“ alisema Benchikha.

Kocha huyo aliyerejea nchini akitokea kwao kushiriki mafunzo ya siku tano ya kuongeza ujuzi, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kujiandaa kwenda kuishangilia timu hiyo kwa ajili ya kuwashangaza Waarabu hao.

„Nawaomba mashabiki wa Simba msiogope kuja uwanjani, njooni, tumejipanga na tumejiandaa

INAENDELEA UK. 23



## Gamondi afunguka ubingwa Bara bado

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuongoza katika msimamo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara bado ni ngumu na ana wasiwasi wa kupata pointi zote sita kutoka kwa Simba na Azam FC.

Yanga inajiandaa kukutana na Azam FC keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi amewakata wachezaji wake kupambana kuvuna pointi tatu katika kila mechi watakayocheza kuanzia mchezo dhidi ya Azam FC ili kuhakikisha wanaendelea kujiimarisha kileleni na kujiweka kwenye nafasi nzuri za kuwania ubingwa.

Gamondi alisema licha ya kuongoza ligi lakini bado ana michezo mingine migumu iliyopo katika hatua za lala salama na imetokana na wapinzani wao kujiimarisha.

Kocha huyo alisema ili kujiweka salama wanatakiwa kuvuna pointi tatu katika kila mechi kwa ajili ya kujiweka kwenye mazingira mazuri na kwao wana-

INAENDELEA UK. 23




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >